View metadata, citation and similar papers at core.ac.uk
brought to you by CORE
provided by Digital Library of Open University of Tanzania

# ATHARI ZA LUGHA NYINGINE KWENYE MIZIZI YA MANENO YA LUGHA YA KISAMBAA

**CLOTILDA WILLIAM MAHIMBO**

**TASNIFU ILIYOWASILISHWA KWA AJILI YA KUTIMIZA SEHEMU YA MASHARTI YA KUTUNUKIWA SHAHADA YA UZAMILI YA KISWAHILI YA CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA**

**2019**

# UTHIBISHO

Aliyeweka sahihi hapa chini amethibitisha kuwa amesoma tasnifu hii inayoitwa ***Athari za lugha nyingine kwenye mizizi ya maneno ya lugha ya Kisambaa,*** naanapendekeza kuwa ikubaliwe na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania katika kukamilisha masharti ya shahada ya Uzamili katika Kiswahili Isimu M.A (Kiswahili) ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.



**Dkt. Dunlop Ochieng**

**(Msimamizi)**

Jumanne, 9 Julai 2019.

Tarehe

## HAKIMILIKI

Tasnifu hairuhusiwi kuiga au kunakili kwa njia yoyote ile, iwe kazi nzima au sehemu ya tasnifu hii, isipokuwa kwa shughuli halali kwa ajili ya utafiti, kujisomea au kufanya marejeo ya kitaaluma bila ya kibali cha maandishi cha kutoka kwa mwandishi au Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

# TAMKO

Mimi Clotilda William Mahimbo, nathibitisha kuwa kazi hii ni yangu mwenyewe halisi na haijawahi kutolewa na haitatolewa katika chuo kikuu kingine chochote kwa ajili ya kutunikiwa shahada nyingine yoyote.

………………………….

Sahihi

………………………….

Tarehe

# TABARUKU

Naitabaruku kazi hii kwa familia yangu, Mume wangu kipenzi Daudi Lloyd Siwale kwa kunitia moyo, kunishauri, na kunisaidia kwa hali na mali mpaka kumaliza kazi hii. Pia watoto wangu wapendwa, natambua kazi kubwa walio ifanya kwa ajili yangu.

## SHUKRANI

Kwanza kabisa napenda kumshukuru Mungu kwa kunipa uhai na afya njema katika kipindi chote cha maisha na katika masomo yangu hadi kuweza kuikamilisha kazi hii.

Pili, shukrani zangu za pekee zimwendee msimamizi wangu Dkt. Dunlop Ochieng kwa kunisimamia vyema katika kazi yangu na kunipa ushauri na maoni mbalimbali yaliyo nisaidia kukamilisha kazi hii.

Tatu, nawashukuru wahadhiri wangu wote wa shahada ya Uzamili, wamenipa maarifa mengi katika taaluma ya lugha, Dkt N. Ligembe, Dkt Z. Elisifa, Dkt H. Jilala, Dkt H. Simpasa na Dkt O. Mohamed pamoja na wanafunzi wote wa M.A (Kiswahili) kwa ushirikiano mzuri, kushauriana, kutiana moyo, na kwa kusoma pamoja na kwa kupeana maoni mbalimbali. Mungu awabariki sana.

Vilevile, natoashukrani zangu za kipekee kwa wazazi wangu wapendwa, Mr William Mahimbo na Bibi Clementina Mgaya kwakunipatia malezi bora, kunisomesha, kunishauri na kunitia moyo katika kipindi chote cha maisha na masomo yangu. Nawashukuru pia wachungaji wangu Askofu Elhuruma swai na Mkewe Marry Swai, Mch Joseph Onesma na Mkewe Marry Onesmo na Mch Bachuba na Mkewe Tusekelege Asajile kwakuniombea na kunitia moyo kipindi chote cha masomo yangu. Mungu awabariki sana. Pia nawashukuru wadogo zangu, Augustino, Nicodemus, Mercy na dada yangu Beatrice William Mahimbo, na rafiki zangu kwa kunipa ushauri, kuniombea na kunitia moyo.Mafanikio ya tasnifu hii yamehusisha

mchango wa watu mbalimbali, ila nimetaja wachache kwani si rahisi kuwataja wote. Wengine wote ambao sijawataja na mmehusika kwa namna moja au nyingine mchango wenu nauthamini mno. Mungu awabariki.

## IKISIRI

Utafiti huu unahusu Athari za lugha nyingine kwenye mizizi ya maneno ya lugha ya Kisambaa. Utafiti umeongozwa na nadharia ya Mofolojia Leksika. Data za utafiti huu zilikusanywa kutoka Wilaya ya Lushoto, kata ya Kwesimu. Lengo kuu la utafiti huu ni kuchunguza athari za lugha nyingine kwenye mizizi ya maneno ya lugha ya Kisambaa. Malengo mahsusi ya utafiti huu ni; Kubainisha mizizi ya maneno ya lugha ya Kisambaa iliyoathiriwa na lugha nyingine; Kueleza athari za lugha nyingine kwenye mizizi ya maneno ya lugha ya Kisambaa; Kubaini mambo yaliyosababisha Lugha nyingine kuathiri mizizi ya maneno ya lugha ya Kisambaa.

Mtafiti alitumia mbinu za hojaji na mahojiano katika ukusanyaji wa data. Sampuli ya watafitiwa 32 ilihusishwa kwa njia ya usampulishaji nasibu na usampulishaji kusudio, kwa kuzingatia kigezo cha umri, jinsia na elimu. Tafiti mbalimbali zilizofanywa katika kuchunguza vipengele mbalimbali katika sarufi ya lugha ya Kisambaa kwa ujumla si katika kuangalia athari za lugha nyingine kwenye mizizi ya maneno ya lugha ya Kisambaa. Matokeo ya utafiti huu yamedhihirisha kwamba mizizi ya maneno ya lugha ya Kisambaa inaweza kuathiriwa na lugha nyingine zinazotumika pamoja . Pamoja na hayo vilevile utafiti huu umebainisha kuwa athari hazitokei kiholela zipo sababu/mambo yanayosababisha athari hizo kutokea na pia utafiti huu umebainisha mbinu za kutumia ili kukabiliana na athari za lugha nyingine kwenye mizizi ya maneno ya lugha ya Kisambaa.

# YALIYOMO

UTHIBISHO ........................................ ii

HAKIMILIKI ........................................ iii

TAMKO ........................................ iv

TABARUKU ........................................ v

SHUKRANI ........................................ vi

IKISIRI ........................................ viii

ORODHA YA MAJEDWALI ........................................ xiii

VIFUPISHO ........................................ xiv

**SURA YA KWANZA** ........................................ 1

1.0 UTANGULIZ WA JUMLA ........................................ 1

1.1 Utangulizi ........................................ 1

1.1.1 Taaluma ya Mofolojia kwa Muhtasari ........................................ 1

1.1.2 Maathiriano ya Lugha ........................................ 2

1.2 Usuli wa Tatizo ........................................ 1

1.3 Tatizo la Utafiti ........................................ 6

1.4 Tamko la Utafiti ........................................ **Error! Bookmark not defined.**

1.5 Malengo ya Utafiti ........................................ 7

1.5.1 Lengo Kuu ........................................ 7

1.5.2 Malengo Mahsusi ........................................ 7

1.6 Maswali ya Utafiti ........................................ 8

1.7 Umuhimu wa Utafiti ........................................ 8

1.8 Mipaka na Mawanda ya Utafiti ........................................ 9

1.9 Hitimisho ........................................ 10

**SURA YA PILI** ........ 11

**2.0 MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA MKABALA WA KINADHARIA** ........ 11

2.1 Utangulizi ........ 11

2.2 Mapitio ya Kazi Tangulizi Mbalimbali Kuhusu Mada ........ 11

2.3 Aina za Mizizi ........ 13

2.4 Tabia ya Mizizi ya Maneno ........ 15

2.4.1 Sifa za Mzizi ........ 16

2.4.2 Muundo wa Mzizi ........ 17

2.4.3 Maumbo ya Mizizi ........ 17

2.4.4 Mzizi na Dhana Nyingine ........ 18

2.4.5 Mzizi na Uambishaji ........ 18

2.4.6 Mzizi na Unyambulishaji ........ 19

2.4.7 Mzizi na Viambishi ........ 20

2.4.8 Upachikaji wa Viambishi Katika Mzizi wa Kitenzi ........ 23

2.4.9 Mizizi Kufuatwa na Viambishi ........ 23

2.4.10 Mizizi Kutanguliwa na Viambishi ........ 24

2.4.11 Athari za michakato ya kimofofonolojia kwenye mzizi ........ 25

2.5 Tofauti baina ya Mzizi na Shina ........ 26

2.6 Vitenzi ........ 28

2.7 Nomino ........ 29

2.8 Pengo la utafiti ........ 30

2.9 Kiunzi cha Nadharia ........ 31

2.10 Hitimisho ........ 33

**SURA YA TATU** ........ 34
**3.0 MBINU ZA UTAFITI** ........ 34
3.1 Utangulizi ........ 34
3.1.1 Utafiti wa Uwandani ........ 34
3.1.2 Utafiti wa Maktabani ........ 34
3.2 Eneo la Utafiti ........ 35
3.3 Populesheni Lengwa ya Utafiti ........ 35
3.4 Sampuli na Usampulishaji ........ 36
3.4.1 Sampuli ........ 36
3.4.2 Usampulishaji ........ 38
3.5 Aina za Data ........ 40
3.5.1 Data za Msingi ........ 40
3.5.2 Data za Upili ........ 40
3.6 Mbinu za Kukusanya Data ........ 41
3.6.1 Mahojiano ........ 41
3.6.2 Hojaji ........ 44
3.6.3 Usomaji na Uchambuzi wa Nyaraka ........ 45
3.7 Mbinu za Uchambuzi wa Data ........ 45
3.7.1 Mkabala wa Kimaelezo ........ 46
3.7.2 Mkabala wa Kiidadi ........ 46
3.8 Vikwazo vya Utafiti ........ 46
3.9 Hitimisho ........ 47
**SURA YA NNE** ........ 48
**4.0 UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA DATA** ........ 48

4.1 Utangulizi ........................................................................................ 48

4.2 Uwasilishaji na Uchambuzi ............................................................ 48

4.2.1 Athari za Lugha Nyingine Kwenye Mizizi ya Maneno ya Lugha ya Kisambaa ........................................................................................ 49

4.2.2 Mambo yaliyosababisha Lugha nyingine kuathiri mizizi ya maneno ya lugha ya Kisambaa ........................................................................................ 59

4.2.3 Mbinu za Kutumika Ili Kuweza Kukabiliana na Athari za Lugha Nyingine Kwenye Mizizi ya Maneno ya Lugha ya Kisambaa ...................................... 63

4.3 Kupotea kwa Mizizi ya Maneno ya Kisambaa .............................................. 66

4.4 Umuhimu wa Kuhifadhi Mizizi ya Maneno ya Lugha ya Kisambaa ............ 67

4.5 Hitimisho ........................................................................................ 68

**SURA YA TANO** ........................................................................................ 69

**5.0 MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO** .............................. 69

5.1 Utangulizi ........................................................................................ 69

5.2 Muhtasari ........................................................................................ 69

5.3 Matokeo ya Utafiti ........................................................................................ 72

5.4 Mafanikio ya Nadharia ........................................................................................ 74

5.5 Mchango wa Utafiti ........................................................................................ 75

5.6 Mapendekezo ........................................................................................ 76

5.7 Hitimisho ........................................................................................ 77

**MAREJEO** ........................................................................................ 78

**VIAMBATANISHO** ........................................................................................ 84

## ORODHA YA MAJEDWALI

Jedwali 2.1: Mifano ya Mizizi Huru ........................................................................ 14

Jedwali 2.2: Mifano ya Mizizi Tegemezi................................................................. 15

Jedwali 2.3: Viambishi Katika Lugha ya Kisambaa ................................................. 23

Jedwali 2.4: Mifano ya Mizizi Kufuatwa Na Viambishi Kwenye Kisambaa ........... 24

Jedwali 2.5: Mifano ya Mizizi Kutanguliwa na Viambishi Kwenye Kisambaa ........ 24

Jedwali 2.6: Mifano ya Mzizi Kutanguliwa na Kufuatiwa na Viambishi Kwenye Kisambaa ......................................................................................... 25

Jedwali 2.7: Vitenzi Katika Lugha ya Kisambaa ...................................................... 29

Jedwali 3.1: Sampuli ya Watafitiwa Kwa Kuzingatia Kigezo czha Umri ................. 39

Jedwali 4.1: Mizizi Katika Lugha ya Kisambaa ....................................................... 55

Jedwali 4.2 Mizizi Katika Lugha ya Kizigua.......................................................... 58

## VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| + | Pamoja na |
| = | Ni sawa na |
| KE | Wanawake |
| LOT | Languages of Tanzania |
| ME | Wanaume |
| Na. | Namba |
| T | Kitenzi |
| TUKI | Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili |

# SURA YA KWANZA

# 1.0 UTANGULIZI WA JUMLA

## 1.1 Utangulizi

Sura hii inakusudia kueleza maana ya mofolojia kwa muhtasari kwa kuwa utafiti unafanyika katika eneo la taaluma ya mofolojia hivyo itasaidia kujenga msingi wa uelewa wa utafiti. Sura hii pia imeangalia usuli wa tatizo, tamko la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, mipaka na mawanda ya utafiti na hitimisho.

## 1.2 Usuli wa Tatizo

### 1.2.1 Taaluma ya Mofolojia kwa Muhtasari

Massamba na wenzake (2003:7), wanasema kuwa ni tawi la isimu ambalo huchunguza maneno na aina za maneno. Na uchunguzi huo unahusu vipashio husika na taratibu zinazotumika katika uundaji wa maneno katika lugha. Wanaendelea kusema kuwa vipande vinavyounda maneno ndivyo hubeba maana ya msingi katika maneno husika.Na vipande hivyo ndivyo viini vya maneno ambayo huitwa mizizi.

Matinde (2012:94), anasema kuwa ni kiwango cha lugha ambacho hushirikiana na viwango vingine yaani fonolojia, sintaksia na semantiki) katika kuijenga lugha. Anaendelea kusema kuwa ni taaluma inayochunguza maumbo na muundo wa maneno katika lugha mahsusi. Ni kiwango cha sarufi ya lugha ambacho huchanganua maumbo ya maneno katika lugha husika.

Mgullu (1999: 94), anasema kuwa mofolojia ina jukumu kubwa la kuyachunguza maneno ili kuyaelewa maumbo yake yalivyo.

Na tunapoongelea maumbo ya maneno yanayochunguzwa na kushughulikiwa na mofolojia, maumbo hayo ya maneno yana vipengele vitatu muhimu ambavyo ni mizizi, viambishi na mashina.

Katika utafiti huu jukumu la mofolojia la kuchunguza maumbo ya maneno limeshughulikiwa kwa maana kwamba nimechunguza kipengele cha mizizi ya maneno ambacho ni kipengele kimojawapo kwenye maumbo ya maneno yanayochunguzwa na mofolojia. Kwa kuchunguza athari za lugha nyingine kwenye mizizi ya maneno ya lugha ya Kisambaa katika kijiji cha Mshelemle, Wilaya ya Lushoto, Mkoa wa Tanga.

Pia ufafanuzi kuhusu dhana ya mzizi, aina, sifa, maumbo/sura ya mizizi, tabia za mizizi ya maneno, mzizi na dhana nyingine umetolewa na kuelezewa kwa kina.

### 1.2.2 Maathiriano ya Lugha

Kuathiriana kwa lugha ni suala ambalo haliwezi kuepukika, lugha huweza kuathiriana kutokana na mwingiliano kati ya lugha mbili au zaidi zilizo tofauti na ni vigumu kuziepuka athari hizo na athari hizo huchangia kudidimiza lugha ya jamii husika. Mwingiliano huu hutokea kutokana na lugha zaidi ya mbili kutumika katika mawasiliano ya kila siku kwani ni vigumu sana kwa jamii moja kutumia lugha moja katika mawasiliano, (Mekacha 2011), anasema kwamba lugha moja huathiriwa kutokana na muktadha wa matumizi yake.

Msanjila (2003), anaeleza kuwa "Tangu zamani dunia imetawaliwa na mwingiliano wa jamii ambao umekuwa wa hiari au wa kulazimisha".
Ullmani (1963), anaeleza kuwa hakuna kitu duniani kinachoweza kubakia katika hali ileile daima "Nothing is perfectly static". Anaeleza kwamba kila lugha, neno, sauti, au lahaja zinaweza kubadilika kutokana na sababu mbalimbali kama vile mwingiliano wa jamii.

Katika jamii kuna kuwepo na mchanganyiko wa watu na huwa na lugha zao tofauti tofauti japokuwa panatakiwa pawepo na lugha teule inayowaunganisha watu hao, kama ilivyo kwa Tanzania lugha teule ni Kiswahili kwa kuwa Tanzania ni nchi yenye lugha nyingi sana. Mwingiliano wa wanajamii wa lugha hizo hupelekea kujitokeza kwa tofauti mbalimbali katika viwango vya lugha (yaani kiwango cha fonolojia, mofolojia, sintaksia na semantiki) katika lugha hizo kwa sababu maneno ya lugha nyingine huingia katika lugha nyingine, kwa kuwa kila lugha ina muundo na sifa zake. Na kwa ujumla maneno katika jamii huonyesha uhusiano uliopo kati ya lugha husika na jamii yake. Kama wanavyoeleza Mekacha (2011) na Radford na wenzake (2002) kwamba kuna uhusiano kati ya jamii na lugha yake na kwamba jamii inaweza kuchambuliwa kupitia lugha na kinyume chake.

Pride na Holmes (1972), wanasema kuwa mojawapo ya mambo yanayosababisha mabadiliko ya lugha ni athari za kutoka nje ya lugha husika. Wanaendelea kusema kuwa mabadiliko husababishwa na kuingiliana kwa jamii.

Kwa hiyo kutokana na msingi huu ninakubaliana na mawazo ya wataalam hawa kuhusu athari za mwingiliano wa lugha. Kutokana na mantiki hii ninaona ipo haja ya kuchunguza athari za lugha nyingine kwenye mizizi ya maneno ya lugha ya Kisambaa, ambayo ndiyo lugha mama kwa Wasambaa na ndio huwaunganisha Wasambaa, ambapo kwa ufahamu wangu eneo hili bado halijachunguzwa na watafitiwa wengine.

Mawazo yote ya wataalamu hawa yamenipa mwanga wa kuweza kupata ruwaza endapo lugha ya Kisambaa imeathirika au haijaathirika kutokana na kutumika pamoja na lugha nyingine.

Wasambaa ni mojawapo ya jamii kutoka Mkoa wa Tanga, kwa kuwa Mkoa wa Tanga kuna makabila mbalimbali kama Wadigo, Wabondei, Wazigua. Wasambaa ni wenyeji wa Wilaya ya Lushoto na pia katika Wilaya hii wanaishi watu wanaozungumza lugha nyingine kama Wapare wanaozungumza Kipare na Wambugu wanaozungumza Kimbugu. Kusambaa kwa jamii hii katika milima ya Usambara ambalo ni eneo linaloitwa Shambalai ambalo limetapakaa milima, ndio chanzo cha jamii hii kuitwa Wasambaa. Jamii hii inasemekana kupanuka nyakati za karne ya 17 na 19, kwa wakati huo asilimia 90% ya wakazi wa Lushoto ni Wasambaa, huzungumza lugha ya Kisambaa, Kishambala au Kishambaa. Coulmas (2005) anafafanua kuwa, lugha ni alama ya utambulisho wa jamii, hupendwa kutumiwa kama ishara ya mshikamano, hubainisha aina ya watu wanaotumia lugha hiyo kupitia lugha yao. Anaendelea kufafanua kuwa aina yetu ya uongeaji hutubainisha kuwa sisi ni nani, tumekulia wapi, msimamo wetu katika maisha na tunataka kutambuliwa kupitia jamii gani. Wasambaa hutambulika kutokana na

majina ya koo zao na hutambuana kutokana na majina ya ukoo. Alama maarufu ya Koo za Kisambaa ni majina yanayoanza na She- kama Shekiangilo, Shekimwei, Shembilu. Jamii hii hujishughulisha na kilimo na ufugaji. Majina mengine yanayotumika kutambulisha Wasambaa ni Shambala na Shambaa. Katika mgawanyo wa lugha za kibantu Guthrie (1971), amekiweka Kisambaa katika kundi la G.20.

Rugemalira na Muzale (2008), wanasema kuwa lugha ya Kisambaa inakadiriwa kuwa na wazungumzaji 565,276 ambayo ni makadirio yaliyofanywa chini ya Mradi wa Lugha za Tanzania (Languages of Tanzania Project – LOT). LOT wanaonyesha kuwa lugha ya Kisambaa ni mojawapo kati ya lugha kubwa kumi na tano (15) nchini Tanzania zenye wazungumzaji wengi. Hata hivyo, Rugemalira na Muzale (2008) weshatajwa, wanaeleza kuwa idadi ya wazungumzaji wa lugha fulani nchini Tanzania si ya kuaminika kwani sensa zinazofanywa hazihusu lugha ama za kabila fulani.

Kisambaa ni lugha ambayo imefanyiwa utafiti na watafiti kutoka sehemu mbalimbali duniani, hivyo kukifanya Kisambaa kuwa mojawapo ya lugha za Kibantu zilizoko katika maandishi. Watafiti hao ni kama vile Roehl (1911), Nurse (1979), Odden (1982), Yukawa (1984), Besha (1985) na Peterson (2008), Habibu (2011) na Abel (2012). Watafiti hawa wamefanya uchunguzi wa sarufi ya lugha hii kifonolojia, kimofolojia, kisemantiki, na kisintaksia. Lengo la wataalamu hawa ya kuchunguza Sarufi ya lugha ya Kisambaa ni ili kuonyesha upekee wa lugha hii, na kuionyesha jinsi lugha hii ilivyo kifonolojia, kimofolojia, kisintaksia na kisemantiki. Masuala mbalimbali yaliyofanyiwa uchunguzi na watafiti hao ni msamiati wa Kisambaa,

sauti za Kisambaa (konsonanti na irabu), vitenzi, njeo, ngeli, sentensi za kisambaa, uambatizi katika vitenzi vya kisambaa, toni, uandishi wa Kamusi ya Kisambaa, muundo wa kirai kitenzi katika lugha ya kisambaa na matumizi ya majina ya ukoo katika utambulisho wa jamii ya wasambaa.

Vipengele hivyo hapo juu ndivyo ambavyo vimefanyiwa uchunguzi katika lugha ya Kisambaa, hata hivyo vipo vipengele vingine mbalimbali ambavyo havijafanyiwa uchunguzi katika lugha hii, vipengele hivyo ni pamoja na Mizizi ya Maneno ya Lugha ya Kisambaa. Hivyo basi utafiti huu umejikita kuelezea na kubainisha Mizizi ya Maneno ya Lugha ya Kisambaa.

### 1.3 Tamko la Tatizo la utafiti

Utafiti huu unakusudia kuchunguza athari za lugha nyingine katika mizizi ya maneno ya lugha ya Kisambaa. Kwa kuwa mizizi ni kipengele muhimu katika lugha ambacho hujitokeza katika maumbo ya maneno. Na pia kwakawaida lugha nyingi za ulimwengu huwa zina mizizi. Hata hivyo, mizizi hubeba maana ya neno na huwa na umuhimu wa kimaana katika maneno yote ya lugha, na kitu kinachojitokeza wazi katika lugha ni maneno. Hivyo utafiti huu umechunguza athari za lugha nyingine katika mizizi ya maneno ya lugha ya Kisambaa kwa kuwa suala hili ni tatizo kubwa kwani huweza kusababisha mizizi ya maneno ya lugha hii kutoweka na kupelekea vizazi vijavyo katika jamii hii kutojua mizizi ya maneno yao, kwa hiyo kutokana na hili utafiti huu umeonyesha athari hizo ili kuweza kuwasaidia wazawa wa jamii hii kukabiliana na athari hizo na kutunza kumbukumbu za mizizi ya maneno yao.

Mzizi ni mojawapo kati ya vitu vya muhimu ambavyo hutazamwa katika lugha. Na ni msingi muhimu katika uundaji wa maneno, japokuwa si maarufu kama neno lakini lazima uwepo pale. Hivyo maneno katika lugha hujibainisha kutokana na mizizi iliyoundwa nayo. Maneno katika jamii moja hutofautiana na ya jamii nyingine kutokana na matumizi ya maneno hayo. Hali hii huweza kusababisha athari katika jamii moja na nyingine kwa kuwa ziko tofauti kadhaa zinazojitokeza katika matumizi ya lugha baina ya jamii moja na nyingine. Kwa hiyo, hapana shaka itakubalika kuwa tofauti hizo zinaweza kusababisha athari kwa wanajamii wa lugha husika na kusababisha mikanganyiko. Kutokana na hayo ndipo utafiti huu umejikita katika kuchunguza athari za lugha nyingine kwenye mizizi ya maneno ya lugha ya Kisambaa ili kuwaelimisha watu mbalimbali wanaotumia lugha ya Kisambaa na kurahisisha kukabiliana na suala hili la athari baina ya jamii ya Wasambaa na jamii nyingine.

## 1.4 Malengo ya Utafiti

Katika utafiti huu, kuna lengo kuu na malengo mahsusi yanayohusu mizizi ya maneno ya lugha ya Kisambaa.

### 1.4.1 Lengo Kuu

Lengo kuu la utafiti huu ni kuchunguza athari za lugha nyingine kwenye mizizi ya maneno ya lugha ya Kisambaa.

### 1.4.2 Malengo Mahsusi

Malengo mahsusi ya utafiti huu ni;

i) Kubainisha mizizi ya maneno ya lugha ya Kisambaa iliyoathiriwa na lugha nyingine.

ii) Kueleza athari za lugha nyingine kwenye mizizi ya maneno ya lugha ya Kisambaa.

iii) Kubaini mambo yaliyosababisha Lugha nyingine kuathiri mizizi ya maneno ya lugha ya Kisambaa.

## 1.5 Maswali ya Utafiti

Maswali ya utafiti huu ni;

i) Ni mizizi ipi ya maneno ya lugha ya kisambaa iliyoathiriwa na lugha nyingine?

ii) Ni athari zipi zilizosababishwa na lugha nyingine kwenye mizizi ya maneno ya lugha ya Kisambaa?

iii) Ni sababu zipi zilizopelekea lugha nyingine kuathiri mizizi ya maneno ya lugha ya Kisambaa?

## 1.6 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu ni muhimu kwa viwango vyote vya elimu; elimu ya msingi, sekondari, vyuo vya kati na vya juu. Utafiti huu ni chanzo kimojawapo kizuri cha kuhifadhi data ya taaluma ya mofolojia inayohusu mizizi ya maneno ya lugha ya Kisambaa nchini. Utafiti huu una msaada kwa wanaisimu mbalimbali katika masuala mbalimbali yanayohusu uchambuzi wa mizizi ya maneno. Kazi hii ni rejeo muhimu kwa wanataaluma hasa wa lugha za kibantu, walimu na wanafunzi, na yeyote atakayekuwa na nia ya kufanya utafiti kwenye mizizi ya maneno na utakuwa ni

mojawapo ya chanzo kizuri cha data. Utafiti huu unatambulisha jamii ya Wasambaa pamoja na mizizi ya maneno ya lugha ya Kisambaa na pia utatoa mchango katika kuhifadhi lugha ya Kisambaa, kwa kuwa watumiaji wake wanaelekea kupungua kila siku kwa kuwa wengi hawatumii lugha hii katika mawasiliano yao.

## 1.7 Mipaka na Mawanda ya Utafiti

Mofolojia ni miongoni mwa tawi la taaluma za isimu, taaluma hii hujishughulisha na dhana mbalimbali. Utafiti huu umelenga kuchunguza dhana ya mizizi ya maneno katika lugha ya Kisambaa kwa kuwa ni vigumu kukwepa matumizi ya dhana ya mzizi katika taaluma ya mofolojia.

Kuchunguza mizizi ya maneno ya lugha ni mchakato unaoendelea ambapo kimsingi unapaswa kuhusisha wanaisimu mbalimbali ili kuondoa mkanganyiko uliopo kwenye kipengele hiki muhimu ambacho hujitokeza katika maumbo ya maneno, kwani kipengele hiki huwa kinachanganywa na kipengele cha mashina ya maneno. Johannes (2007), anasema kuwa wataalamu wengine, kwa sababu ya kutokuwepo ubayana wa dhana hizi, hutumia dhana ya mzizi sawa na dhana ya shina. Kwa kuwa watu hukanganyikiwa wasijue ni umbo lipi liitwe mzizi na lipi liitwe shina. Hivyo basi itakuwa ni vyema kama wanaisimu mbalimbali watafanya tafiti mbalimbali ili kuiweka wazi dhana hii na kuifafanua zaidi ili ieleweke kwa watu. Utafiti huu umejikita katika kuchunguza athari za lugha nyingine katika mizizi ya maneno ya lugha ya Kisambaa katika kijiji cha Mshelemle, kata ya Kwesimu katika Wilaya ya Lushoto Tanga.Utafiti huu umefanyika katika sehemu ambayo lugha hii ya Kisambaa inazungumzwa na kutumika yaani Wilaya ya Lushoto Mkoani Tanga.

Mizizi ya maneno haipatikani tu katika lugha hii iliyoteuliwa bali hupatikana katika maneno ya lugha nyingi za ulimwengu. Lakini kutokana na muda wa utafiti lugha moja tu ya Kisambaa imefanyiwa utafiti.

Utafiti umechunguza mizizi ya maneno ya lugha ya Kisambaa katika kitenzi na nomino japokuwa mzizi ni dhana inayohusu kategoria mbalimbali za maneno kama vile vivumishi na vielezi na siyo kitenzi na nomino tu. Licha ya ukweli kuwa maneno mengine kama vivumishi, na vielezi bado havijachunguzwa, utafiti huu umeshughulikia mizizi ya maneno katika vitenzi na nomino pekee.

## 1.8 Hitimisho

Katika sura hii, fasili ya mofolojia imeelezwa kwa muhtasari kwa kuwa utafiti huu umefanyika katika taaluma ya mofolojia.

Licha ya hilo, pia umeelezwa usuli wa utafiti, tamko la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, mipaka na mawanda ya utafiti na hitimisho na sehemu inayofuata imeshughulikia mapitio mbalimbali ya maandiko**.**

# SURA YA PILI

# 2.0 MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA MKABALA WA KINADHARIA

## 2.1 Utangulizi

Surahii imegawanyika katika sehemu mbili: Sehemu ya kwanza inaangalia mapitio ya maandiko mbalimbali yanayohusu mizizi ya maneno ya lugha. Sehemu ya pili inaonyesha nadhariaitakayotumika kufafanua mizizi ya maneno ya lugha ya Kisambaa katika utafiti huu.

## 2.2 Mapitio ya Kazi Tangulizi Mbalimbali Kuhusu Mada

Dhana ya mzizi imejadiliwa na wanazuoni mbalimbali kama tutakavyoona katika sura hii.Mapitio ya maandiko mbalimbali yanayohusu mizizi ya maneno katika lugha mbalimbali kama kiingereza na Kiswahili, lugha hizi zimerejelewa ili kuonyesha mizizi ya maneno katika lugha nyingine za binadamu. Kiswahili kinawakilisha lugha nyingine za kibantu ili kuonyesha upekee wa lugha za kibantu. Kila lugha ya kibantu inaweza kuwa na upekee wake katika mizizi ya maneno.

Tafiti hizo na mapitio ya maandiko mbalimbali ama yameeleza tu kwa ujumla mizizi ya maneno, na jinsi inavyokuwa kwenye neno na maana inayobeba na kutolea mifano ya jumla inayoonyesha mizizi ya maneno. Lengo la kutumia tafiti zilizotangulia ni kufahamu mapengo ya tafiti hizo ili kutoa fursa ya kufanyiwa uchunguzi zaidi.

Lugha mbalimbali duniani huwa na vijenzi maalumu vinavyounda maneno. Katika lugha tenganishi(kama Kichina na Kivietinamu),kwa mfano, maneno huundwa kwa

neno moja moja bila kuchanganyika na viambishi. Katika lugha ambishi-bainishi kama Kiswahili na Kisambaa, maneno huundwa kwa mfuatano bayana wa mofimu. Mofimu hizo huwa na maana na mizizi hudhihirika wazi bila kuchanganyika na viambishi. Mofimu katika lugha ambishi changamani huwa na uamilifu zaidi ya mmoja. Hivyo,mofimu moja kwa mfano inaweza kuwakilisha njeo, nafsi, kauli na kadhalika. Aidha, katika lugha kama Kiarabu na Ciruu, mofimu huchopekwa ndani ya mzizi na huwa vigumu kutenganisha mzizi na viambishi (Mgullu, 1999, Massamba,2004).

Lugha yoyote ile huwa na vipengele vitatu muhimu ambavyo hujitokeza katika maumbo ya maneno. Vipengele hivyo muhimu ni mizizi, viambishi na mashina. Vipengele hivi huonyeshwa jinsi vilivyo kimaumbo na kiuamilifu.Na vipengele hivi ndivyo viambajengo vya maneno katika lugha.Maneno katika lugha zote huundwa kwa mzizi, viambishi na shina.

Kwa kawaidalugha nyingi za ulimwengu huwa zina mizizi kwenye maumbo ya maneno. Ukweli ni kwamba mzizi wa neno hutumika kuelezea neno na ni kitengo cha maana cha neno. Aidha inaonekana kwamba mizizi mingi ya maneno huundwa na konsonanti pekee na hutanguliwa na viambishi.

Crystal (1987:267), anasema mzizi ni umbo-msingi la neno ambalo haliwezi kuchanganuliwa tena katika sehemu nyingine ndogo bila kupoteza(uamilifu) na utambulisho wake (wa kisemantiki).

Kihore na wenzake (2004), wanakubaliana na Crystal (1987), kuwa mzizi ni umbo-msingi la neno ambalo haliwezi kuchanganuliwa tena katika sehemu nyingine ndogo bila kupoteza (uamilifu na) utambulisho wake kisemantiki.

Rasinski(2008), anasema mzizi ni sehemu ya neno inayomaanisha kitu fulani.Anaendelea kusema kuwa ni kundi la herufi lenye maana.Pia anaendelea kusema kuwa mizizi mingine huwa sehemu tu ya neno. Naye Hartman (1972), anasema mzizi ni sehemu ya msingi ya neno ambayo ina taarifa ya kileksika na ya kisarufi.Massamba na wenzake(2003:53), wanasema mzizi ni kipengele muhimu ambacho hujitokeza katika maumbo ya maneno ya lugha.

Matinde(2012:108), "mzizi ni mofu ambayo ni muhimu zaidi katika neno na huweza kukaa peke yake kama neno kamili. Aidha, hii ni sehemu ya neno ambayo haibadilikibadiliki. Katika uchanganuzi wa neno, mzizi hauwezi kuchanganuliwa katika sehemu nyingine ndogo bila kupoteza uamilifu na maana yake.

Kiango (2000) anakubaliana na Bauer (1983) kuwa mzizi wowote au shina lolote laweza kuwa ni kiini. Kiini ni umbo lolote la neno ambalo viambishi vya aina yoyote vyaweza kupachikwa, kwa maana kwamba kiini cha neno huweza kuambishwa.
Hivyo basi, mzizi ni kiini cha neno na ni sehemu ya neno ambayo maneno mengine huundwa kutoka kwayo.

## 2.3 Aina za Mizizi

Kihore na wenzake (2004:63), wanakubaliana na Mgullu (1999), Matinde (2012), Mohamed (1993), Massamba (2003), Good (2005) na TUKI (1996), kuwa kwa

kawaida lugha nyingi ulimwenguni huwa zina mizizi ya aina mbili nayo ni mizizi funge(tegemezi), yaani ile isiyoweza kusimama yenyewe kama neno na huundwa na kitenzi na hutegemea viambishi vingine ndani ya neno moja, maneno mengi ya Kibantu huundwa na mizizi funge (Massamba na wenzake (1999). Mizizi huru, ni ile mizizi isimamayo yenyewe kama neno na hubeba/huundwa na nomino inayoifanya isiweze kugawanyika zaidi na huwa na maana iliyo kamili. Ugawaji huu wa mizizi ni wa kimofo-semantiki, hii ni kusema umezimgatia kigezo cha kimaumbo na cha kimaana.

Lugha ya Kisambaa kama zilivyo lugha nyingine za Kibantu na zisizo za kibantu ina mizizi. Katika lugha ya Kisambaa kuna mizizi huru na mizizi tegemezi kama ilivyo katika lugha nyingine. Mizizi inapatikana katika maneno na si mahali pengine. Hivyo, sehemu ya kuweza kupata mizizi ya maneno ya Kisambaa ni katika maneno ya Kisambaa. Katika utafiti huu nimekusanya mizizi huru na tegemezi.

**Jedwali 2.1: Mifano ya Mizizi Huru**

| Na | Mzizi | Neno | Maana |
|---|---|---|---|
| 1. | Bada | Bada | Ugali wa muhogo |
| 2. | Fii | Fii | Mvi |
| 3. | Mame | Mame | Mama |
| 4. | Mani | Mani | Majani |
| 5. | Tate | Tate | Baba |
| 6. | Wau | Wau | Dada |
| 7. | Ngoto | Ngoto | Kondoo |
| 8. | Zisho | Zisho | Jicho |
| 9. | Si | Si | Nzi |
| 10. | Zina | Zina | Jina |

**Jedwali 2.2: Mifano ya Mizizi Tegemezi**

| Na | Mzizi | Neno | Maana |
|---|---|---|---|
| 1. | to- | Toa | Piga |
| 2. | kuj- | Kuja | Kula |
| 3. | im- | Ima | Lima |
| 4. | ghu- | Ghuwa | Chukua |
| 5. | ond- | Onda | Tafuta |
| 6. | shek- | Sheka | Cheka |
| 7. | shez- | Sheziga | Cheza |
| 8. | zeng- | Zenga | Jenga |
| 9. | zim- | Zima | Zima |
| 10. | ush- | Usha | Ondoa |

## 2.4 Tabia ya Mizizi ya Maneno

Massamba na wenzake (2003:53), (weshatajwa) wanasema mzizi kama umbo la msingi lina tabia moja kuu, nayo ni ile ya kutobadilikabadilika katika maneno yote yanayohusiana nalo.

Wanaendelea kusema kuwa maumbo mengine yote yanayobaki katika kila neno huweza kubadilikabadilika na huongezea tu maana za ziada zinahusiana na maana ya msingi inayobebwa na mzizi.

Kihore (2011:25), anakubaliana na Mgullu (1999:102), kuwa mzizi ni umbomsingi, hivyo umbo husika huwa halibadiliki katika mazingira yoyote yale ya uchanganuzi, kwa maana ya kuwa umbo la mzizi ni moja tu na haliongezeki wala kupungua, unavyoviongeza kwenye mzizi huwa ni viambishi tu na havibadilishi umbo la mzizi na pia ndio hubebana na vipashio vingine vyote vyenye kuhusiana nacho katika utokeaji wake kiisimu, wenyewe ukiwa ni chimbuko la michakato yote yenye kuhusiana na utokeaji huo. Kwa mfano:

1) Mizizi ya maneno ya Kiswahili

**i)-imb-** katika neno

- Ana**imb**a
- Ata**imb**a
- Uli**imb**wa

ii) **-sana** katika neno (a) **sana**

2) Mizizi ya maneno ya Kisambaa

**-hak-** katika neno

- Nta**hak**a
- Ne**hak**e
- Nza**hak**a

3) Mizizi ya maneno ya Kiingereza

- **-book** katika neno (a) **book**shop
- **-window**katika neno (a) **window**-clean
- **-hard** katika neno (a) **hard**ship

### 2.4.1 Sifa za Mzizi

Johannes (2011), anakubaliana na Mgullu(1999) na Matinde(2012), kuwa mzizi una sifa zifuatazo; Mzizi huweza kusimama peke yake kama neno kamili. Kwa mfano; baba, ng'ombe, Pia mzizi huweza kuunda neno jipya. Mzizi huwa hauchanganuliwi zaidi na pia mizizi huwa haubadiliki. Mzizi ni mofu muhimu zaidi kuliko mofu zingine zote katika neno,kwa maana kwamba mofu zingine kama viambishi hupata maana wakati zinapotumiwa pamoja na mzizi.

### 2.4.2 Muundo wa Mzizi

Mzizi huundwa na konsonanti pekee, lakini yapo maneno ya lugha nyingine ambayo mzizi hupachikwa irabu, mfano lugha ya kiebrania, mfano; gdl – largness – gadol. Johannes (2011), anasema kuwa mzizi ni kiini cha neno kinachoishia na konsonanti.

Mfano: Katika lugha ya Kiswahili;

i) a**ch** + a

ii) so**m** +a

iii) o**g** + a

iv) cho**t** + a

v) ongo**z** + a

Mfano: Katika lugha ya Kisambaa

i) ghe**nd** + a - tembea

ii) a**gh** + a - potea

iii) ka**w** + a - chelewa

iv) iva**n** + a - kubali

v) i**mb** + a - imba

### 2.4.3 Maumbo ya Mizizi

Mgullu (1999), anasema kuwa mizizi ya maneno ina sura mbalimbali. Kwa hali kama hii mizizi haiwezi kufananishwa na kitu kimoja tu. Kwa hiyo, njia sahihi ya kuelewa mzizi ni ile ya kuutafuta mzizi katika muktadha wa maneno mbalimbali yanayotokana na mzizi huo.

Mgullu (1999), keshatajwa anakubaliana na Matinde (2012), kuwa mizizi ina maumbo tofauti tofauti kama vile, Mizizi inayofanana na fonimu, kwa mfano; katika lugha ya Kiswahili katika maneno yafuatayo: ku**f**a – {**f**}, ku**l**a – {**l**}. Mizizi ambayo ni maneno kamili, kwa mfano; dada, mwalimu, tena. Mizizi inayoundwa na fonimu zaidi ya mbili, kwa mfano; pika- (-pik-), cheza – (-chez-). Na mizizi inayofanana na silabi, kwa mfano; mtu – m + **tu** – {**tu**}, mto – m + **to** – {**to**}.

### 2.4.4 Mzizi na Dhana Nyingine

Katika mofolojia ni vigumu kukwepa matumizi ya dhana ya mzizi. Katika dhana mbalimbali kwenye mofolojia dhana ya mzizi hutajwa.

### 2.4.5 Mzizi na Uambishaji

Massamba (2004), anaieleza dhana ya uambishaji kuwa ni utaratibu wa kuweka kiambishi kabla, kati na baada ya mzizi. Hivyo, katika fasili hii dhana ya mzizi imetajwa tayari, hii inadhihirisha ukweli kuwa katika mofolojia ni vigumu kukwepa matumizi ya dhana ya mzizi.

Johannes (2011), anasema kuwa kuna baadhi ya mizizi ya maneno huweza kufanyiwa uambishaji na baadhi ya mizizi ya maneno ambayo haiwezi kufanyiwa uambishaji ambayo ni maneno huru kama vile ‘baba’-, kwa kuwa mzizi huu hauwezi kuchanganuliwa zaidi, kwa maana hiyo viambishi vya aina yoyote haviwezi kuwa sehemu ya mzizi wa neno huru.

Mfano wa uambishaji kwenye Kisambaa

i) Itanga – mu – itang – o

ii) Kunda – u – kundish – o

iii) Eleka – mb- elek – o

### 2.4.6 Mzizi na Unyambulishaji

Kapinga (1983), anafafanua "unyambulishaji" kutokana na neno "nyumbua au nyambua", anasema kwamba kunyambua ni kurefusha kitu kama mpira. Kwa ujumla, unyambulishaji ni tendo la kuambatanisha viambishi kwenye mzizi ili kulirefusha na kupata neno lenye maana ingine.

Kahigi (2009), anafafanua unyambulishi kutokana na vinyambulishi kuwa ni mchakato unaozalisha maneno au kuongeza maana fulani kwenye mzizi au shina. Mnyambuliko hujitokeza kwa namna mbili. Namna ya kwanza, ni kutenganisha kitenzi katika sehemu mbili yaani mzizi wake na kiambishi tamati. Namna ya pili, ni kurefusha mzizi huu kwa kutumia viambishi fulani, kwa mfano katika neno "pika", mzizi ni –pik- na – a ni kiambishi tamati. Ukiweka kiambishi -i- kati ya mzizi na kiambishi tamati, unapata "pik - i – a, hivyo maana inabadilika kuwa kauli ya kutendea.

Mfano wa unyambulishaji kwenye Kisambaa

i. Toza- tozwa, tozeka, tozana, tozeshwa

ii. Ima - imwa, imika, imiwa, imisha, imishwa

iii. Toa - toighwa, kutoighwa, toana

Kaoneka (2009), anaeleza kuwa katika lugha ya Kishambala unyambulishaji hubadili mofolojia ya kitenzi ambacho huwa na athari kisintaksia na kisemantiki. Mwandishi

anasisitiza kuwa ingawa unyambulishaji wa vitenzi katika lugha ya Kishambala unafanana na wa lugha nyingine za Kibantu, lugha hii ina upekee wake ambao unautofautisha na lugha nyingine. Kwanza vitenzi vyake huweza kuambikwa viambishi nyambulishi vitatu hadi vinne tofauti na lugha nyingine kama vile Kinyambo.Rugemalira (1993)

Wana wa - za - boh - ez - an – a makui.

Waghoshi wa -za - ish -i -iz -an – a ngoto.

Chanzo: (Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili, Kioo cha lugha, Juz.11, 2003:60).

### 2.4.7 Mzizi na Viambishi

Massamba na wenzake (2003), wanasema viambishi ni mofimu zinazoambatanishwa kwenye mzizi wa neno ili kuwakilisha hali au dhana mbalimbali zinazofungamana na neno pamoja na mofimu hizo. Viambishi hujitokeza katika lugha mbalimbali za ulimwengu. Katika lugha ya Kiswahili viambishi huweza kujitokeza tu mwanzoni au mwishoni mwa mzizi. Kwa hiyo, viambishi huambikwa kwenye mizizi, kama vile tend-a, ji-we, vi-gogo, katika mifano hii vipashio vilivyoandikwa kwa chapa iliyokoza ni viambishi.

Katamba (1993) anakubaliana na Bloomfield (1888), Whitney (1989) na Goldsmith (1990), kuwa kuna viambishi vya aina kuu mbili kutokana na mkabala wa Mofolojia Leksika, viambishi visivyo na athari(neutrol affixes) na viambishi vyenye athari(non-neutrol affixes). Viambishi visivyo na athari ni viambishi ambavyo havina athari

kwenye mzizi au shina la kitenzi na havisababishi mabadiliko yoyote ya kimofofonolojia. Kwa mfano kiambishi {-ji} katika neno mchekeshaji, msomaji, {-e} katika neno kiumbe, upinde .Viambishi vyenye athari ni viambishi ambavyo vina athari katika mzizi au mashina ya maneno katika lugha na ambavyo vikipachikwa katika mzizi au shina vinaathiri kwa namna fulani konsonanti au irabu ya shina au mzizi huo. Viambishi hivyo vyenye athari ni {-i}, {u} na {-o}, (Wesana-Chomi, 2003 na Kihore na wenzie 2003). Mfano katika neno soma likipachikwa kiambishi {o} kwenye mzizi linabadilika na kuwa somo hivyo maana ya neno inakuwa imebadilika. Kwa hiyo viambishi hivi vyenye athari vinaweza kusababisha mabadiliko ya kisemantiki, kifonolojia na kimofolojia au yote mawili yaani kimofofonolojia. Mabadiliko haya yanaweza kutokea hata kwenye shadda, kiimbo, sauti au mofimu fulani ya mzizi au shina.

Katamba keshatajwa na wanazuoni hao hapo juu wamethibitisha kuwa athari ya viambishi wakati mwingine hujitokeza kwenye viambishi vyenyewe vinapopambanishwa na mzizi au shina la neno. Sauti mojawapo katika viambishi kinachohusika inaweza kuathiriwa na kupata umbo jingine. Pia athari hizi huweza kujitokeza katika lugha za kibantu zenye tabia kama lugha ya Kiswahili.

Mfano: Katika lugha ya Kiswahili

T MZIZI KINOMINISHI = NOMINO UNDE (NOMINO ZINAZOUNDWA

1. Soma som- + -o = somo
2. Jenga jeng- + -o = jengo

3. Cheka chek- + -i = ucheshi
4. Andika andik- + -i = mwandishi
5. Linda lind- + -i = mlinzi

Mfano: Katika lugha ya Kisambaa

T MZIZI KINOMINISHI = NOMINO UNDE(NOMINO ZINAZOUNDWA

1. Soma som- + -o =somo
2. Zenga zeng- + -o =zengo
3. Sheka shek- + -i =ucheshi
4. Andika andik- + -i =mwandishi
5. Linda lind- + -i =mlinzi

Katika mifano hiyo hapo juu inaonyesha jinsi ambavyo viambishi{-o , -i} vilivyosababisha athari za kimofofonolojia katika mizizi ya vitenzi. Kwenye data yetu katika (1) na (2) huonyesha matokeo ya kitendo fulani. Mathalani matokeo ya kujenga ni jengo na ya kusoma ni kupata somo yaani jambo la kujifunza. Na katika (3), (4) na (5) imesababisha athari kutokana na sauti ya mwisho katika mzizi wa kitenzi, sauti / k/ imebadilika na kuwa /š/ baada ya kupachikwa kinominishi {-i} na sauti /d/ imebadilika na kuwa /z/.

Kwa hiyo, vipo viambishi vyenye nguvu ya kuathiri konsonanti ya mwisho ya mashina au mizizi ya vitenzi mara tu vinapopachikwa mwishoni mwa mizizi ya vitenzi na kusababisha mabadiliko kwenye mizizi na shina la neno.

### 2.4.8 Upachikaji wa Viambishi Katika Mzizi wa Kitenzi

Viambishi vingi hutumika katika kuunda kitenzi, kwa maana kwamba viambishi huweza kupachikwa kabla au baada ya mzizi na kuunda kitenzi kama vile viambishi vya nafsi, wakati, hali. Kwa mfano neno **anatupikia** limeundwa na viambishi vifuatavyo;

**a** – kiwakilishi cha nafsi,

**na-** kiwakilishi cha wakati,

**tu-** kiwakilishi cha nafsi

**pik-** mzizi wa kitenzi.

**i-** kinyambulishi cha hali ya kufanyia

**a**-kiambishi tamati

Kitenzi cha Kisambaa kimeundwa na mzizi na viambishi mbalimbali, yaani viambishi awali na viambishi tamati, viambishi hivyo kimofolojia vina dhima mbalimbali. Jedwali hapo chini linaonyesha viambishi vinavyopatikana katika vitenzi vya Kisambaa.

**Jedwali 2.3: Viambishi Katika Lugha ya Kisambaa**

| N | Vitenzi | Viambishi awali | Viambishi tamati |
|---|---|---|---|
| | Azadikiwa | **a + za** | **iw + a** |
| **ii** | Wamuusha | **wa + mu** | **a** |
| **iii** | Azaghuliwa | **a + za** | **iw + a** |
| **iv** | wazamuusha | **wa + za + mu** | **a** |
| **v** | Azakundwa | **a + za** | **w + a** |

### 2.4.9 Mizizi Kufuatwa na Viambishi

Kiambishi huweza kupachikwa mwishoni mwa mzizi, katika lugha ya Kiswahili neno huweza kuundwa kwa kupachika kiambishi kimoja au viambishi kadhaa,

mwishoni mwa mzizi. Kwa mfano; (a) panga – pang –**a ,** pang**- ik - a, (**b**)** uma **-** um **– a,** um**- iz – w - a,** katika mifano hii vipashio vilivyoandikwa kwa chapa iliyokoza ni viambishi vilivyopachikwa mwishoni mwa mzizi.

**Jedwali 2.4: Mifano ya Mizizi Kufuatwa Na Viambishi Kwenye Kisambaa**

| Na | Neno | Mzizi | Viambishi | Maana |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Zuta | zut- | a- | Vuta |
| 2 | Haka | hak- | a- | 0ga |
| 3 | Iha | ih- | a- | Lipa |
| 4 | Ogoha | ogoh- | a- | Ogopa |
| 5 | Toza | toz- | a- | Kamata |

### 2.4.10 Mizizi Kutanguliwa na Viambishi

*Mzizi* huweza *kutanguliwa na kiambishi kimoja au viambishi vingi. Kwa mfano; kiti – **ki** – ti, jicho – **ji** – cho, katika mifano hii vipashio vilivyoandikwa kwa chapa iliyokoza ni viambishi vilivyopachikwa mwanzoni mwa mzizi.*

**Jedwali 2.5: Mifano ya Mizizi Kutanguliwa na Viambishi Kwenye Kisambaa**

| Na | Neno | Viambishi | Mzizi | Maana |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Utana | u- | Tana | Uzuri |
| 2 | Uvizu | u- | Vizu | Uvivu |
| 3 | Ubada | u- | Bada | Ubaya |
| 4 | Uvuvi | u- | Vuvi | Uvuvi |
| 5 | Utii | u- | Tii | Utii |

#### 2.4.10.1 Mzizi Kutanguliwa na Kufuatiwa Na Viambishi

Katika lugha ya Kiswahili, kama ilivyo katika lugha za Kibantu zote, kuna utaratibu mwingine wa mpangilio wa maneno ambao unaruhusu baadhi ya viambishi kutangulia mzizi, na baadhi yake vikafuatia mzizi katika umbo hilohilo moja. Hii ina

maana kwamba katika maumbo ya namna hiyo mzizi unakuwa katikati ya viambishi vya kushoto na kulia.

Kwa mfano;

a) **m- ta- tu-** pelek **-a _______ m-ta-tu-** pelek –**e -a,**

b)**tu- ta-** on- **an -a _________ tu-ta-**on- **an -a,**

*Katika* mifano *hii vipashio vilivyoandikwa kwa chapa iliyokoza ni viambishi vilivyopachikwa mwanzoni na mwishoni mwa mzizi, na vilivyopigiwa mstari ni mizizi.*

**Jedwali 2.6: Mifano ya Mzizi Kutanguliwa na Kufuatiwa na Viambishi Kwenye Kisambaa**

| Na | Neno | Viambishi | Mzizi | Viambishi | Maana |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Mghuzi | m- | ghuz- | i- | Mnunuzi |
| 2 | Mdishi | m- | dish- | i- | Mpishi |
| 3 | Muimbi | mu- | imb- | i- | Mwimbaji |
| 4 | Mulimi | mu- | lim- | i- | Mlimaji |
| 5 | Mlosi | m- | los- | i- | Mzungumzaji |

### 2.4.11 Athari za michakato ya kimofofonolojia kwenye mzizi

Johaness (2011), anasema kuwa michakato ya kimofofonolojia huweza kuathiri mizizi na kuchukua umbo jingine ambalo ni la nje.

Mfano: Katika lugha ya Kiswahili

i) Pend- a - m –penz - i

ii) Pand- a - m- panz - i

iii) Suk - a - m- sus - i

iv) Pik - a - m – pish – i

## 2.5 Tofauti baina ya Mzizi na Shina

Johannes (2011:23), anakubaliana na TUKI (1990:53), kuwa shina, ni sehemu ya neno ambayo inaundwa na mzizi na viambishi/ kiambishi angalau kimoja au na muambatano wa mizizi katika maneno ambatani.

Johannes (keshatajwa), anaendelea kusema kuwa, shina katika Sarufi ya Kiswahili ni mzizi unaoambatana na viambishi vya mnyambuliko, naye Katamba (1993:45), anasema kuwa mashina yanaweza kuwa kiini endapo tu yanatumika katika muktadha wa uambatishi.

Mifano ifuatayo inatuonyesha mizizi na shina kwenye Kiswahili na Kisambaa

**i) Mzizi** **Shina**

- chung- chunga
- chez- cheza
- ham- hama
- sif- sifu

**ii) Mzizi** **Shina**

- kin- kina
- hon- hona
- uy- uya
- aw- awa

Kihore na wenzie (2004:89-93), wanaeleza kuwa, dhana ya mzizi na shina huweza kutofautishwa kwa utaratibu wa uambishaji ambao ama unaweza kuunda au kutounda neno jipya, wametoa mifano ifuatayo ili kushadidia hoja yao;

**Mfano wa 1**

- walk - walks - walked
- kick - kicks - kicked

a) show - shows - showed

Katika mifano hiyo hapo juu kwa mujibu wa Kihore na wenzie hayo ni mashina ya maneno kwa kuwa maana ya msingi ni ileile hivyo hakuna neno jipya lililoundwa.

**Mfano wa 2**

- piga
- **pig**-w-a
- a-ta-**pig**-a
- a-li-**pig**-a

Katika mfano huu umbo **piga** katika 2(a) **ni shina,** lakini katika 2 (b), (c), na (d) maneno hayo hayajaundwa na shina piga bali mzizi **pig-**( au kwa maana nyingine hayahusiani na uambishaji wa Kisarufi), 2 (b) ina kiambishi –**w-** cha kauli ya utendwa kati ya konsonanti ya mwisho ya mzizi na irabu ishilizi, viambishi vyote vya kauli vinahusiana na mofolojia ya mnyambuliko/uambishaji-nyambulishi wa vitenzi, hii ina maana kwamba viambishi vya kauli hubadili mwelekeo wa maana ya msingi ya neno tofauti na mofolojia ya uambatishi.(Polome, 1967; Kahigi, 2003; Rugemalira, 2005).

Kwa hiyo, tunaweza kusema kuwa, dhana ya mzizi na shina ni dhana ambazo hutofautiana na kila dhana ina mpaka wake. Johannes (2011), keshatajwa anasema

kuwa dhana ya shina na mzizi zina sifa zake pambanuzi ambazo huweka mpaka baina ya dhana hizi; mzizi una sifa zake pambanuzi zinazoutofautisha na shina ambazo ni huhusika na uundaji wa neno jipya, hupambanuliwa na mofolojia ya mnyambuliko, ni kiini cha neno kinachoishia na konsonanti, ni sehemu ya neno isiyobadilika na pia ni sehemu ya neno isiyoweza kuchanganuliwa zaidi. Na sifa pambanuzi za shina ni; shina ni sehemu ya neno ambayo haiwezi kuunda neno jipya, hupambanuliwa na mofolojia ya uambatishi, pia ni kiini cha neno kinachoishia na irabu na ni umbo la neno lenye mzizi angalau kiambishi kimoja.

## 2.6 Vitenzi

Nkwera (1978), anadai kuwa kitu kinachojionyesha wazi kabisa katika lugha ni maneno, hivyo maneno ya kategoria mbalimbali, vitenzi vikiwa vimojawapo. Vitenzi vina dhima kubwa katika lugha.

Massamba (2004), anakubaliana na Nkwera (1978), kuwa vitenzi ni maneno yanayoarifu jambo ambalo hufanywa na jina. Kwa mfano; mtoto <u>anaiba</u>, mama <u>anapika</u> wali, Neema <u>amepigwa</u> leo.

Katika mifano hii maneno yaliyopigiwa mstari yanaeleza au yanaarifu jambo ambalo linafanywa na jina. Nkwera (1978), anaendelea kusema kuwa, “kitenzi” ni neno ambalo linabeba vitu vingi ndani yake. Vitu hivi ni viambishi mbalimbali ambavyo vinasaidia kuunda kifungutenzi.

Charwi (2013:62), anasema vitenzi vya kibantu vinaweza kugawanywa katika makundi tofautitofauti kwa kutumia kigezo cha kisemantiki au kisintaksia. Kwa

mfano; kisemantiki kuna vitenzi vinavyoelezea tendo katika hali fulani mfano kujua, kuwa nakadhalika. Vitenzi vinavyoelezea mwendo kwa mfano; kimbia, tembea, vya matendo kama vunja, kata na kadhalika. Kisintaksia – vitenzi hugawanywa kwa kuzingatia uhitaji wa wahusika katika kukamalisha tendo hilo, kwa mfano; kuna vitenzi vinavyohitaji mhusika mmoja tu yaani mtenda, mfano, mtoto amelala, vinavyohitaji wahusika wawili, baba amenunua gari, Juma amechukua kikombe, na vinavyohitaji wahusika watatu, mwalimu amempa mwanafunzi daftari, kaka ameweka kitabu mezani. (Chanzo: Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili, Kioo cha lugha, Juz.11, 2003:60).

Lugha ya Kisambaa ina vitenzi vya aina mbalimbali na vitenzi hivi huishia na –**a**, kama inavyoonyesha katika jedwali 1.2.

**Jedwali 2.7: Vitenzi Katika Lugha ya Kisambaa**

| Na. | Vitenzi vya Kisambaa | Kiswahili |
|---|---|---|
| I | Kunda | penda |
| II | Kuja | kula |
| III | Sheka | cheka |
| IV | Ghosha | lala |
| V | Gonad | andika |

## 2.7 Nomino

Masebo J.A na mwenzake (2002), wanasema nomino ni maneno yanayotaja vitu, viumbe, hali au matendo ili kuviainisha na kuvitofautisha na vitu vingine. Wanaendelea kusema kuwa nomino zaweza kuwa majina ya viumbe vyenye uhai kama vile wanyama, ndege, mimea, watu, wadudu n.k. Au majina ya viumbe visivyo

hai kama viti, meza, maji, udongo, kisu n.k na majina ya matendo mfano uchezaji, ufugaji, uogeleaji, uimbaji n.k.

Matinde (2012) anakubaliana na Habwe & Karanja (2004) weshatajwa, kuwa nomino ni neno ambalo hutaja mtu, kitu, hali, mahali, dhana na tendo.

Lugha ya Kisambaa kama zilivyo lugha nyingine ina aina mbalimbali za nomino kama inavyoonyesha hapa chini;

| Nomino za Kisambaa | | Kiswahili |
|---|---|---|
| i) | Tuni | kisu |
| ii) | Mesho | macho |
| iii) | Ziko | jiko |
| iv) | Mame | mama |
| v) | Zumbe | Mungu |

## 2.8 Pengo la utafiti

Wataalamu mbalimbali wameongelea suala la mwingiliano wa lugha ambao ni William (1913), Corder (1967), Mohamed (2001), Idarus (2005), Mbaab (2007) na Athuman (2015). Wanazuoni hawa walifanya uchunguzi na kugundua kuwa lugha zinapoingiliana husababisha athari kwenye lugha husika na kuleta mabadiliko kwenye maneno kwa kuzalisha maneno mapya, muundo wa sentensi na mabadiliko kwenye sauti, kutokana na haya kufanyiwa uchunguzi na wanazuoni hawa mtafiti alichunguza na kugundua kuwa hakuna aliyejadili athari za lugha nyingine kwenye mizizi ya maneno ya lugha nyingine. Hivyo basi, utafiti huu ulikusudia kuongeza uwanja mpana wa maarifa kwa kutafiti mwingiliano wa lugha uliosababisha athari

kwenye mizizi ya maneno ya lugha ya Kisambaa, ambapo utakapomalizika utakuwa chanzo kizuri cha data katika taaluma ya Mofolojia.

## 2.9 Kiunzi cha Nadharia

Jilala (2016:60), anasema nadharia ndio msingi mkuu wa kuweza kuelezea jambo fulani ili liweze kukubalika, kuaminika na kufanyiwa kazi na watu wa jamii husika ama taaluma ya fani husika. Anaendelea kusema kuwa kila fani ina dira inayoiongoza fani hiyo katika uchunguzi, uchambuzi na ufafanuzi wa fani ama taaluma ya fani husika. Ndiyo sababu kuna nadharia za isimu, fasihi, siasa, uchumi,sosholojia, na utawala.

Uteuzi wa nadharia itakayotumika hutegemea nia ya mtafiti, jambo linalotafitiwa na hali ya lugha inayotafitiwa. Kwa hiyo, utafiti huu wa mizizi ya maneno ya lugha ya Kisambaa unatumia nadharia ya Mofolojia leksika, Mofolojia leksika ni nadharia zalishi na nyambulishi inayotambua kiwango cha mofolojia kama kiwango mahususi cha lugha, ambayo ni taaluma ya isimu inayoelezea uhusiano uliopo baina ya mofolojia na fonolojia na hufafanua jinsi mofolojia na fonolojia zinavyohusiana katika mchakato wa uambishaji na/ au unyambulishaji, kwamba wakati wa uambishaji au unyambulishaji kuna sauti zinaathirika ama kwenye mzizi/shina la neno au kwenye kiambishi chenyewe na hivyo kusababisha mabadiliko ya kiumbo (Katamba, 1993).

Nadharia hii imejengwa katika misingi ya mkabala unaoitambua mofimu kama kipashio cha msingi cha kiuchanganuzi (Lieber, 1990, 1992). Nadharia ya mofolojia

leksika inaeleza kwamba mofolojia kama sehemu ya lugha imepangwa katika mfuatano wa ngazi kimsonge (Kiparsky, 1982, Katamba, 1993, Macmahon 2000, Katamba na Stonham, 2006). Hii ina maana kwamba viambishi (mofimu) vinavyopachikwa katika mizizi ya neno hupangwa kidarajia.

Kimsingi nadharia hii inaonyesha uhusiano wa maumbo ya maneno na sheria zinazodhibiti maumbo hayo. Nadharia ya mofolojia leksika hutambua viwango viwili vya kanuni ambavyo ni kanuni leksika ambazo huhusika katika kuunda neno kubalifu kileksika na kanuni kirai ambazo hutenda kazi baada ya neno kuundwa. Nadharia ya mofolojia leksika imejengwa katika mihimili mbalimbali kama vile kanuni ya ngazi leksika, kanuni ya mzunguko kamili, kanuni ya kufuta mabano, kanuni ya ufinyu wa sifa na kanuni ya kuhifadhi muundo.

Kwa kuwa utafiti huu unachunguza ruwaza za kimofolojia za mizizi ya maneno, hivyo uchanganuzi wa data unaongozwa na nadharia hii ya mofolojia leksika. Katika utafiti huu nadharia hii imeongoza kwenye uchambuzi wa malengo yote ya utafiti huu.
Lengo la kwanza, nadharia hii imeongoza kwa kuchambua na kuonyesha namna ambavyo mizizi ya kisambaa imeathirika na kupata mabadiliko ya kiumbo (mofolojia) na mabadiliko ya kimatamshi (kifonolojia) na kuwa na muelekeo wa kiswahili kiasi cha kueleweka kwa mtu yeyote yule hata ambaye siwajamii ya Wasambaa. Lengo la pili, nadharia hii imeongoza kwa kuchambua na kuonyesha namna ambavyo lugha ya kiswahili imesababisha lugha ya kisambaa kupoteza ladha yake halisi pamoja na kutokukua na kuendelea kwa lugha ya kisambaa kutokana na

kupotea kwa maumbo na matamshi halisi ya maneno yake. Lengo la tatu, nadharia hii imesaidia kuonyesha mambo yaliyosababisha lugha nyingine kuathiri mizizi ya maneno ya lugha ya kisambaa.

Msingi wa kuteuliwa kwa nadharia hii ni madai ya mhimili wa kanuni ya ngazi leksika kwamba maneno huundwa na vipashio mbalimbali na vipashio hivyo vimepangwa katika ngazi kimsonge. Vipashio hivyo huunganishwa hatua kwa hatua na kujenga vipashio vikubwa zaidi. Hivyo basi, nadharia hii ya mofolojia leksika inatumika katika kubainisha na kufafanua ruwaza za kimofolojia za mizizi ya maneno ya lugha ya Kisambaa. Maneno ya lugha yameundwa kwa mizizi hivyo huweza kuchanganuliwa kimofolojia. Kwa hakika nadharia hii imemwezesha na kumsaidia mtafiti katika kufikia malengo yake ya utafiti huu.

## 2.10 Hitimisho

Sura hii imejikita katika upitiaji wa maandiko mbalimbali ambayo yametumika katika kujenga hoja madhubuti yaliyofanya utafiti huu uwe muhimu kufanyika.Pili, kiunzi cha nadharia kilichoongoza utafiti huu kimejadiliwa.

# SURA YA TATU

## 3.0 MBINU ZA UTAFITI

### 3.1 Utangulizi

Sura hii inahusu mbinu za utafiti zilizotumika katika ukusanyaji wa data za utafiti huu.Kothari (2014), anasema kuwa mbinu za utafiti ni taratibu zilizotumika katika ukusanyaji wa data za utafiti. Pia sura hii imebainisha eneo la utafiti ambalo mtafiti amekusanya data aliyoifanyia uchambuzi juu ya mizizi ya maneno ya lugha ya Kisambaa. Kutokana na malengo ya utafiti, utafiti huu umetumia mbinu ya utafiti wa uwandani na mbinu ya utafiti wa maktabani.

#### 3.1.1 Utafiti wa Uwandani

Katika utafiti huu, data zilikusanywa moja kwa moja kwa watafitiwa katika maeneo yaliyoteuliwa ambayo ni Lushoto Mkoa wa Tanga.

#### 3.1.2 Utafiti wa Maktabani

Utafiti huu umefanyika katika kupitia kazi tangulizi katika maktaba za Chuo Kikuu cha Dar-es-salaam na TATAKI(MAKAVAZI) na LOT na Maktaba ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. Mbinu hii ya utafiti wa maktabani imemsaidia mtafiti kupata data za uhakika za upili juu ya mizizi ya maneno ambazo zilipatikana kwenye kazi tangulizi za wanazuoni wa lugha mbalimbali za asili, Kiingereza na Kiswahili. Mtafiti alizipata data hizi za upili kwa kusoma na kwa kuzichambua kazi hizo tangulizi.

## 3.2 Eneo la Utafiti

Utafiti huu wa kuchunguza Athari za lugha nyingine kwenye mizizi ya maneno ya lugha ya Kisambaa umefanyika katika Wilaya ya Lushoto katika kata ya Kwesimu, japokuwa imeelezwa awali kuwa kuna maeneo mbalimbali ambako lugha hii ya Kisambaa inazungumzwa. Sababu za kuchagua eneo hili ni pamoja na urahisi wa kufikika, na pia ndiko wanakoishi Wasambaa wanaozungumza Kisambaa asilia na ni eneo ambalo lililopo mbali na mjini hivyo wapo wazungumzaji ambao hawajaathiriwa sana na Kiswahili, hivyo ni rahisi kupata data kuhusu mizizi ya maneno inayotambulisha maneno ya Kisambaa yenye maana. Hata hivyo, kuna uwezekano wa kuwepo waliopata athari za Kiswahili kutokana na elimu, vyombo vya habari, na pia kuwepo kwa njia za usafiri kutokana na kukua kwa miji ambapo watu wanatoka sehemu moja kwenda nyingine ambavyo vimechangia kwa kiasi kikubwa katika ukuzaji wa matumizi ya lugha ya Kiswahili. Ralf (1987), anaelezea kuwa mojawapo ya sababu za kubadilika kwa lugha ni kutokana na kukua kwa miji, uhamiaji na maendeleo ya viwanda. Hata hivyo athari hizo si sawa na zile walizozipata wazungumzaji wa Kisambaa waishio mjini.

## 3.3 Populesheni Lengwa ya Utafiti

Populesheni ni kundi la watu lenye kufafana katika mambo kadhaa kama vile utamaduni ambamo sampuli huchukuliwa (Kombo na Tromp,2006). Enon (1999:13), anaeleza kwamba populesheni ni vitu au watu ambao ambao kwao mtafiti anatarajia au amepata data ya utafiti. Populesheni lengwa ya utafiti itahusisha jamii nzima, makundi ya watu, au vitu vingine ambavyo kwavyo mtafiti amevihusisha kama chanzo cha data. (Cooper, 1989, Vans, 1990).

Hivyo katika utafiti huu populesheni lengwa ni jumla ya wakazi wote wanaoishi katika Wilaya ya Lushoto ambao ndio walionipatia data ya utafiti huu.

## 3.4 Sampuli na Usampulishaji

### 3.4.1 Sampuli

Sampuli ni idadi ya watafitiwa maalumu ambayo huteuliwa na kundi kubwa la watu kwa ajili ya kutoa taarifa zinazochunguzwa na mtafiti(Enon, 1998).

Sampuli ni seti ya washiriki (watu) huchaguliwa kutoka kwenye idadi kubwa kwa lengo la utafiti (Webster, 1985). Hivyo, sampuli ni wawakilishi ama viwakilishi vya watafitiwa wote ambayo huteuliwa na mtafiti ili vimpatie data lengwa za kukamilisha utafiti husika.

Mtafiti yoyote yule anapofanya utafiti wa kitaaluma hulazimika kuteua sampuli ndogo ambayo itawakilisha jamii nzima ili kutimiza madhumuni mahsusi ya utafiti wake. Kwa kawaida mtafiti huchagua na kuteua sampuli ya watafitiwa kwa kuzingatia vigezo mbalimbali alivyoviweka mtafiti mwenyewe kwa kuzingatia malengo ya utafiti, aina ya utafiti, umri, jinsi nakadhalika.

Sampuli inaweza kuwa ni sampuli nasibu, sampuli takabishi, sampuli kusudio/lengwa, sampuli tajwa, sampuli fursa. Katika utafiti huu sampuli nasibu, sampuli kusudio/lengwa ndizo zilizo kutumika.

#### 3.4.1.1 Sampuli Nasibu

Ni aina ya sampuli ambayo inatoa nafasi sawa kwa watafitiwa wote kuwepo katika kutafitiwa ambapo majina ama namba huwekwa kwa watafitiwa kisha watafitiwa kuchagua.

Mbinu hii ilichaguliwa na mtafiti kwa sababu husaidia kupunguza upendeleo katika kutafuta watafitiwa na huwezesha kasoro kurekebishwa. Mbinu hii imetumika katika vijiji vya kata ya Kwesimu ambapo watafitiwa wachache walihojiwa ambao ni vijana 6 wazee 6 na wanafunzi 4. Mbinu ya usampulishaji iliyotumika kupata sampuli hii ni usampulishaji nasibu.

#### 3.4.1.2 Sampuli Kusudio

Ni sampuli ambayo watafitiwa huchaguliwa kwa sababu maalumu kulingana na utafiti ili kupunguza upendeleo ambapo kila mtafitiwa huwa na fursa sawa ya kuwemo katika sampuli.

Sampuli hii ilichaguliwa kwa sababu inamfanya mtafiti kwa makusudi kabisa kuteua mtafitiwa hivyo kuongeza uhakika wa data kwani mtafitiwa huwa na sifa zinazohitajika. Pia inampa mtafiti nafasi ya kuweza kujiridhisha na data alizozipata. Sampuli hii imetumika kwa kuteua wazee na wasomi katika maeneo mbalimbali. Mbinu ya usampulishaji iliyotumika kupata sampuli hii ni usampulishaji kusudio, ambapo wazee 6, walimu 4 na wanafunzi 6.

### 3.4.2 Usampulishaji

Ili mtafiti aweze kupata sampuli husika ni lazima afanye usampulishaji. Kothari, (1990), anasema usampulishaji ni mchakato wa uteuzi wa watafitiwa kutoka katika populesheni lengwa ya utafiti ili wawe sampuli ya utafiti. Aidha si mara zote huteuliwa sampuli kuwakilisha, mara nyingine huchukuliwa sampuli kamili.

Webster, (1985), anasema usampulishaji ni kitendo, mchakato au mbinu ya kuchagua sampuli inayofaa, au sehemu inayowakilisha idadi ya watu kwa lengo la kuamua vigezo au tabia ya idadi ya watu wote.

Katika usampulishaji, kwa kawaida huwezi kuhusisha kila mmoja katika kundi kubwa, kwa sababu hiyo makosa yanaweza kutokea kutokana na tofauti iliyopo katika uwakilishaji wa idadi ya watu katika kundi na kile kinachowakilishwa katika sampuli. Labov, (1972), anasema kuwa ili kuwa ili kuelezea au kuandikia sarufi ya lugha fulani,mtafiti anahitaji kukusanya data kubwa. Data hiyo anaweza kuipata kwa kukusanya mazungumzo ya wazawa wengi na lugha husika kadri inavyowezekana.

Mtafiti ametumia mbinu ya usampulishaji nasibu na kusudio katika utafiti huu. Usampulishaji huu ulimsaidia mtafiti kupata data halisi alizokuwa akizihitaji, data hizo zilimsaidia mtafiti kwenye kukamilisha malengo yake ya utafiti huu ambazo alizipata kwa njia ya mahojiano na hojaji.

Katika utafiti huu, mtafiti ameunda sampuli kwa kuzingatia umri wa watafitiwa ambao wamegawanywa sawasawa kwa kuzingatia umri, katika umri kati ya miaka

15 -75. Mtafiti aliwapanga na kuwaweka watafitiwa wake katika makundi manne ambayo ni miaka 15-30, 30-45, 45-60 na 60-75. Kundi la miaka 15-30 na 30-45 ni kundi la vijana na ni wasomi chuo kikuu cha SEKOMU ambao wanauelewa mkubwa na mzuri kuhusu mizizi ya maneno, kwa hakika kundi hili lilimwezesha na kumsaidia mtafiti kupata data nzuri na za uhakika. Kundi la miaka 45-60 na 60-75 ni kundi wazee na walimu (Mazinde Juu Sekondari) ambalo linajua vizuri lugha asilia ya Kisambaa. Kwa hakika, makundi haya yote yalimsaidia mtafiti kupata data za uhakika. Mtafiti ametumia sampuli hii ili kupata data kubwa. Hata hivyo, idadi ya watafitiwa kama ilivyoonywesha kwenye jedwali inatosheleza kutoa data zilizotakiwa na haita athiri matokeo ya utafiti. Sampuli hiyo itakuwa kama jedwali 3.1 linavyoonyesha hapa chini.

**Jedwali 3.4.1: Sampuli ya Watafitiwa Kwa Kuzingatia Kigezo czha Umri**

| UMRI | MAKUNDI YA WATAFITIWA | IDADI | | |
|---|---|---|---|---|
| | | **ME** | **KE** | **JUMLA** |
| 15 – 30 | Wanafunzi/Vijana | 4 | 4 | 8 |
| 30 – 45 | Walimu/Vijana | 4 | 4 | 8 |
| 45 – 60 | Walimu | 4 | 4 | 8 |
| 60 – 75 | Wazee | 4 | 4 | 8 |
| | | **16** | **16** | **32** |

Jedwali 3.1 linaonyesha jumla ya watafitiwa watakuwa 32. Mtafiti ametumia dodoso pamoja na kufanya mahojiano na watafitiwa. Wazungumzaji hao wamemsaidia mtafiti kupata maneno mengi yenye mizizi. Sababu za kuchukua umri mchanganyiko ni kutaka kuchunguza na kubaini uelewa wa kila kundi kuhusu dhana ya mzizi wa maneno.

## 3.5 Aina za Data

Data katika utafiti ni taarifa zilizokusanywa, zilizopangwa, zilizoonwa, au undwa kwa madhumuni ya uchambuzi ili kuzalisha matokeo ya utafiti wa awali. Na huwakilishwa katika mazingira fulani ili kufanywa kuwa za muhimu/zenye umuhimu.

Utafiti wowote hutegemea data, data katika utafiti hutumika katika kutaja takwimu za utafiti, na ni ukweli ulio wazi. Pia hutumika katika kuwakilisha wazo, ukweli na takwimu. Data lazima ifasiriwe na kupatiwa maana ili iweze kuwa taarifa kamili na hivyo kutumika kuongeza maarifa. Katika utafiti huu tumekusanya data za aina mbili, yaani data za msingi na data za upili.

### 3.5.1 Data za Msingi

Kothari na Garg (2014), wanasema, data za msingi, ni data ambazo zimekusanywa kwa upya na kwa mara ya kwanza na hivyo kutokea kuwa halisi katika tabia. Katika utafiti huu nimetumia data za msingi ambazo zimekusanywa kutoka uwandani.

### 3.5.2 Data za Upili

Kothari na Garg (2014), weshatajwa, wanasema, data za upili, ni data ambazo zilishakusanya na mtu mwingine na ambazo tayari zimekwishapitia katika mchakato wa takwimu. Data hizi za upili juu ya mizizi ya maneno zilipatikana katika kazi tangulizi mbalimbali na maandiko ya machapisho mbalimbali kupitia maktaba za Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam na TATAKI (MAKAVAZI) na LOT na Maktaba ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

### 3.6 Mbinu za Kukusanya Data

Kutokana na mtazamo wa utafiti huu wa kuchunguza Athari za lugha nyingine kwenye mizizi ya maneno ya lugha ya Kisambaa, ukusanyaji wa data ulifanyika kwa kutumia mbinu za mahojiano, hojaji na usomaji na uchambuzi wa kazi tangulizi. Mbinu hizi zimeteuliwa na mtafiti ili zimsaidie mtafiti kupata taarifa za kiutafiti zilizoweza kukidhi mahitaji ya utafiti.

#### 3.6.1 Mahojiano

Kothari (2004), Kombo na Tromp, (2006) wanakubaliana kuwa, mahojiano ni majibizano ya ana kwa ana ambayo huhusisha kuuliza maswali kwa njia ya mazungumzo ya mdomo, au kwa njia ya simu au kwa njia ya barua pepe kati ya watu wawili au zaidi( mtafiti na watafitiwa) ambapo mtafiti huwahoji watafitiwa wake.

Kuna mahojiano ya aina tatu, mahojiano funge, ni mahojiano ambayo majibu yake huwa yamefungwa na hayaruhusu kujieleza. Mahojiano nusufunge, ni aina ya mahojiano ambayo maswali yake mengine huacha mwanya wa kujieleza. Tatu, ni mahojiano yasiyofunge, haya ni mahojiano ya kina yanayotoa uhuru kwa mtafitiwa kujieleza kwa ufasaha kwa kadiri anavyoweza.

Katika kufanya mahojiano na watafitiwa kuna mahojiano rasmi na yasiyo rasmi. Mahojiano rasmi, ni mahojiano ambayo mtafiti anafanya makubaliano na watafitiwa kuhusu muda na mahali pa kukutana, hivyo mtafiti anatakiwa kuwa na maswali ya mwongozo. Mahojiano yasiyo rasmi, ni mahojiano ambayo hayajapangwa rasmi, ambayo mtafiti anaweza kukutana na watafitiwa bila taarifa rasmi.

Mtafiti katika utafiti huu ametumia mahojiano yasiyofunge na ya ana kwa ana na mahojiano rasmi na yasiyorasmi ili kuweza kupata taarifa za kiutafiti zilizowezesha kukidhi malengo ya utafiti. Hivyo mtafiti amefanya mahojiano na watafitiwa huku akiwa na dodoso lenye maswali yaliyowapa watafitiwa uhuru wa kujieleza atakavyo yeye mwenyewe.

Mbinu hii ya mahojiano ilitumiwa na mtafiti kwa sababu ilikuwa na faida nyingi katika utafiti huu. Kwanza, husaidia kupata taarifa za ziada ambazo si rahisi kuzipata kwa kutumia njia ya hojaji. Pili, ilisaidia kupata mawazo na mitazamo mbalimbali ya watafitiwa yaliyomsaidia mtafiti kutafiti zaidi kuhusu maneno, mizizi yake pamoja na maana zake. Tatu, ilimpa mtafiti fursa ya kuona mazingira yanayofaa kutokana na upatikanaji wa watafitiwa na pia mahojiano hayo yaliendeshwa kwa lugha ya Kiswahili na yalifanyika kwa mtu mmoja mmoja.

Katika mbinu hii ya mahojiano, mahojiano yalifanyika kwa njia ya majadiliano pamoja na maswali baina ya mtafiti na watafitiwa, ambapo majibu mazuri yaliyoeleweka yalitolewa na watafitiwa katika maswali yaliyoulizwa na mtafiti, hivyo ilimsaidia mtafiti kupata data halisi. Mahojiano yalifanyika kwa kuongozwa na maswali, ambapo mtafiti aliwauliza maswali wahojiwa kumi na sita kwa kutumia maswali kumi na mbili ambayo yamegawanyika katika sehemu kuu mbili, sehemu A ambayo ni ya taarifa binafsi za msingi za mtafitiwa ambazo ni muhimu kwenye uchanganuzi wa data na sehemu B niliuliza maswali yaliyohusu athari za lugha nyingine kwenye mizizi ya maneno ya lugha ya Kisambaa amapo wahojiwa wote

kumi na sita waliulizwa maswali, kwa kutumia maswali yafuatayo; Je unadhani kuwa mizizi ya maneno ya lugha ya Kisambaa imeathiriwa na lugha nyingine zinazotumika pamoja nayo? (a) ndio (b) hapana. Kama jibu lako ni ndio taja lugha hiyo/hizo. Hapa kila mhojiwa alitoa jibu lake na kutaja lugha iliyoiathiri lugha ya Kisambaa. Swali lingine mtafiti alilowauliza watafitiwa wake, Ni mizizi ipi ya maneno ya lugha ya Kisambaa iliyoathiriwa na lugha nyingine? Taja. Kwenye swali hili kila mhojiwa alitaja mizizi ya maneno ya lugha ya Kisambaa iliyoathiriwa na lugha nyingine.

Swali la tatu ni; Ni athari zipi zilizosababishwa na lugha hizo kwenye lugha ya Kisambaa kutokana na mizizi ya maneno yake kuathiriwa? Eleza, Kila mhojiwa katika swali hili alitaja athari zilizosababishwa na lugha nyingine kwenye lugha ya Kisambaa kutokana na mizizi ya maneno yake kuathiriwa. Swali la nne; Ni sababu zipi zinazopelekea lugha nyingine kuathiri mizizi ya maneno ya lugha ya Kisambaa?, Kila mhojiwa alitoa sababu zilizopelekea athari ya lugha hizo kwenye Kisambaa.
Mtafiti alichagua watafitiwa thelathini na mbili (16) ambao aliwahoji, watafitiwa hao waliteuliwa kulingana na jinsia zao, umri wao, na kiwango chao cha elimu.

Watafitiwa waliohojiwa: Wanafunzi 6, wakike 3 na wakiume 3, wanafunzi hao watateuliwa kwa kuwa wanauelewa juu ya mizizi ya maneno. Wazee 6, wanawake 3 na wanaume 3, wazee hawa waliteuliwa kutokana na uelewa wao wa lugha ya kisambaa. Walimu 4, wakiume 2 na wakike 2, hawa waliteuliwa kwa kuwa walimu wana uelewa mkubwa wa mizizi ya maneno.

### 3.6.2 Hojaji

Ni mbinu inayotumia maswali yanayotayarishwa katika maandishi na kupewa mtafitiwa ili ayajibu kwa maandishi. Kuna aina mbili za hojaji ambazo ni hojaji huru, ambapo mtafitiwa ana uhuru wa kutoa maelezo yake, na hojaji funge ambapo mtafitiwa hana uhuru wa kutoa maelezo na maoni yake (Chava na David, 1981).

Mbinu hii ya hojaji imetumiwa na mtafiti katika utafiti huu kwa sababu imeweza kutumika eneo kubwa kwa wakati mmoja. Pili, inaokoa muda kwani mtafiti si lazima afike moja kwa moja kwa watafitiwa, anaweza kuwatumia hojaji zake. Tatu, mbinu hii hutunza siri kwa hiyo watafitiwa wanapata uhuru wa kujaza wanachokielewa bila wasiwasi. Nne, mbinu hii haina gharama kubwa kwani unaweza kupata data yote inayohitajika katika eneo moja kwa wakati mmoja na kwa gharama nafuu. Pia husaidia kurahisisha ukusanyaji wa data kutoka kwa watafitiwa wengi kwa muda mfupi. Hata hivyo mbinu hii ikitumiwa vizuri haitoi majibu ya upendeleo kwani mtafitiwa anajaza kile anachokifahamu yeye mwenyewe. Mbinu hii ya hojaji inalenga kutupatia data za maneno ya lugha ya Kisambaa, mizizi yake na maana zake.

Mtafiti alichagua vipengele vitatu vya kuchunguza katika mizizi ya maneno ya lugha ya Kisambaa ambavyo ni; kubaini mizizi ya maneno ya lugha ya Kisambaa iliyoathiriwa na lugha nyingine, kubaini lugha iliyoiathiri lugha ya Kisambaa, athari zilizosababishwa na lugha hizo kwenye lugha ya Kisambaa na sababu zilizopelekea lugha nyingine kuiathiri mizizi ya maneno ya lugha ya Kisambaa.

Katika utafiti huu mtafiti aliandaa dodoso yenye sehemu tatu na kila sehemu ina maswali yake ambayo mtafitiwa anatakiwa kuyajibu. Watafitiwa waliojaza dodoso hilo ni (16) na ni wale wanaojua kusoma na kuandika. Mtafiti alifanyia kazi majibu yaliyojibiwa na watafitiwa ili kupata taarifa alizozikusudia. Kila hojaji ilikuwa imegawanyika katika sehemu kuu tatu. Sehemu ya kwanza ilihusu taarifa za msingi za mtafitiwa, ambazo ni muhimu katika uchanganuzi wa data. Sehemu ya pili mpaka ya tatu ilihusu mizizi ya maneno ya lugha ya Kisambaa iliyoathiriwa na lugha nyingine, athari za lugha nyingine kwenye mizizi ya maneno ya lugha ya Kisambaa lugha, na sababu zilizosababisha athari hizo kwenye lugha ya Kisambaa, lengo la sehemu hizi ni kupata taarifa mbalimbali zinazofafanua athari hizo pamoja na sababu za zilizosababisha athari hizo kwenye Kisambaa. Njia hii ya dodoso na ya mahojiano zilimsaidia na kumwezesha mtafiti kupata data zilizo halisi alizokuwa anazihitaji.

### 3.6.3 Usomaji na Uchambuzi wa Nyaraka

Hii ni mbinu ya kukusanya data ambapo mtafiti husoma kazi mbalimbali makatabani hususani zile zinazohusu mada yake ya utafiti. Hivyo, mtafiti alitumia mbinu hii kwa kusoma na kazi tangulizi zilizohusu mizizi ya maneno kwenye lugha mbalimbali za asili, Kiingereza na Kiswahili. Njia hii ilitumiwa na mtafiti kwa kuwa ni chanzo kizuri na cha uhakika cha kupata data. Kwa hakika, njia hii ilimsaidia mtafiti kupata data zilizomsaidia kufikia malengo yake.

## 3.7 Mbinu za Uchambuzi wa Data

Uchambuzi wa data zilizokusanywa kwa njia ya mahojiano na hojaji zilichambuliwa kwa mkabala wa kimaelezo na mkabala wa kiidadi.

### 3.7.1 Mkabala wa Kimaelezo

Mkabala huu wa kimaelezo hutumika katika utafiti wenye lengo la kuelezea tabia ya mtu au kikundi fulani cha watu, na kuelezea hali iliyopo (Kothari, 2004). Mtafiti ametumia mkabala wa kimaelezo kwa kuwa maelezo ndiyo yametumika zaidi katika kuonyesha mizizi na pia taarifa mbalimbali kuhusu mawazo ya watafitiwa juu ya mizizi ya maneno na data nyingi zilizokusanywa zilitolewa kwa njia ya maelezo.
Kwa kutumia maneno, mtafiti amebainisha mizizi iliyopo katika lugha ya Kisambaa. Katika kubainisha maneno hayo ndipo ameweza kutambua aina za mizizi ya Kisambaa na amefafanua aina hizo na zimeelezewa kwa kutumia majedwali, vipashio vinavyoandamana na mizizi hiyo. Pia ameonyesha athari za lugha nyingine kwenye mizizi ya maneno ya lugha ya Kisambaa, sababu za athari na mbinu za kukabiliana na athari hizo.

### 3.7.2 Mkabala wa Kiidadi

Huu ni mkabala unaohusisha mahesabu au takwimu katika utafiti. Mtafiti alitumia mkabala huu wa kiidadi ili kuweka data zilizopatikana katika majedwali na kutafuta asilimia ya data hizo kulingana na jinsi watafitiwa walivyojibu maswali yaliyoulizwa katika hojaji. Na pia kuonesha idadi ya watafitiwa na majedwali yaliyoonyesha mizizi ya maneno ya lugha ya Kisambaa.

## 3.8 Vikwazo vya Utafiti

Wakati wa ukusanyaji wa data zilijitokeza changamoto mbalimbali, changomoto ya kwanza iliyojitokeza ilikuwa ni upatikanaji wa watafitiwa hii ilitokana na kwamba

kilikuwa ni kipindi cha kilimo ambapo watu wengi walikuwa wameenda mashambani, na pia wanafunzi wengi na walimu walikuwa wamefunga shule na kusafiri maeneo mbalimbali ya nchi hivyo ikamuwia vigumu mtafiti kuwapata kirahisi. Pili, imejitokeza katika maswali ya hojali, maswali yalikuwa mengi hivyo baadhi ya watafitiwa walionekana kuwa wazito na wenye muitikio hafifu kumaliza kuzijaza hojaji walizo pewa.

Japokuwa changamoto hizo zilijitokeza wakati wa ukusanyaji wa data hazikuathiri upatikanaji wa data za kutosha na za kuaminika kutoka kwa watafitiwa. Kwani data zilizo kusanywa zilikidhi malengo ya utafiti

## 3.9 Hitimisho

Sura hii imeanza kwa utangulizi wa jumla, imebainisha mbinu za utafiti ambazo ni utafiti wa uwandani na maktabani, imebainisha na kujadili mbinu za ukusanyaji wa data, eneo la utafiti, populesheni lengwa, sampuli na usampulishaji, aina za data na mbinu za uchambuzi wa data.

# SURA YA NNE

# 4.0 UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA DATA

## 4.1 Utangulizi

Sura hii inahusu uwasilishaji na uchanganuzi na ufasiri wa matokeo ya utafiti yaliyopatikana uwandani kuhusu athari za lugha nyingine kwenye mizizi ya maneno ya lugha ya Kisambaa. Watafitiwa walipatikana kwa kutumia usampulishaji nasibu na kusudio. Data zilikusanywa kwa njia ya hojaji na mahojiano. Uchanganuzi wa data umefanywa kwa kutumia njia ya maelezo na majedwali nayo yametumika kwa sehemu baadhi ili kubainisha data zinazohusika.

## 4.2 Uwasilishaji na Uchambuzi

Katika uwasilishaji na uchambuzi wa data ulizingatia malengo ya utafiti ambayo ni lengo kuu na malengo mahsusi na kwa kufuata maswali ya utafiti yanayohusu mizizi ya maneno ya lugha ya Kisambaa. Katika kuwasilisha na kuzichambua data mtafiti alianza na data zilizopo kwenye maandishi ambazo ziliandikwa na watafitiwa na zilizoandikwa na mtafiti kwa kuwasaidia watu wazima ambao hawakuweza kusoma na kuandika na hatimaye mtafiti alimalizia kwa kusikiliza sauti zilizorekodiwa na mtafiti kwa kutumia simu yake. Mtafiti alifanya hivyo ili kuchunguza na kubaini uhalisia na ukweli wa data ambazo zilitusaidia juu ya mada, na uchambuzi ulituwezesha kuunda majedwali yenye takwimu zilizofikia malengo mahsusi ya utafiti huu.

### 4.2.1 Athari za Lugha Nyingine Kwenye Mizizi ya Maneno ya Lugha ya Kisambaa

Lengo kuu la utafiti huu lilikuwa ni kuchunguza athari za lugha nyingine katika mizizi ya maneno ya lugha ya Kisambaa, hivyo data zilitokana na lengo hili pamoja na malengo mahususi ya utafiti huu.

Data zilipatikana kwa njia ya mahojiano na kuchambuliwa kwa njia ya maelezo na jedwali, kutokana na malengo na majibu yaliyopatikana kutokana na maswali ya utafiti, ambayo mtafiti aliwauliza watafitiwa wake, na kila swali lilikuwa na lengo la kupata majibu halisi.

Swali la kwanza, Je unadhani kuwa mizizi ya maneno ya lugha ya Kisambaa imeathiriwa na lugha nyingine zinazotumika pamoja nayo? (a) ndiyo, (b) hapana, kama jibu lako ni ndiyo taja lugha hiyo/hizo. Swali hili lilikuwa ni kutaka kupata lugha iliyoiathiri mizizi ya maneno ya lugha ya Kisambaa. Kutokana na swali hili mtafiti aliwahoji watafitiwa kumi na sita(16) na wote walitoa majibu.

Mhojiwa wa kwanza alisema ndiyo, kuwa mizizi ya maneno ya lugha ya Kisambaa imeathiriwa na lugha nyingine zinazotumika pamoja nayo na aliitaja lugha ambayo imeiathiri mizizi ya maneno ya lugha ya Kisambaa ambayo ni lugha ya Kiswahili.

Mhojiwa wa pili alisema ndiyo, kuwa mizizi ya maneno ya lugha ya Kisambaa imeathiriwa na lugha nyingine zinazotumika pamoja nayo na aliitaja lugha ambayo imeiathiri mizizi ya maneno ya lugha ya Kisambaa ambayo ni lugha ya Kiswahili.

Mhojiwa wa tatu alisema ndiyo, kuwa mizizi ya maneno ya lugha ya Kisambaa imeathiriwa na lugha nyingine zinazotumika pamoja nayo na aliitaja lugha ambayo imeiathiri mizizi ya maneno ya lugha ya Kisambaa ambayo ni lugha ya Kiswahili.

Mhojiwa wa nne alisema ndiyo, kuwa mizizi ya maneno ya lugha ya Kisambaa imeathiriwa na lugha nyingine zinazotumika pamoja nayo na aliitaja lugha ambayo imeiathiri mizizi ya maneno ya lugha ya Kisambaa ambayo ni lugha ya Kiswahili.

Mhojiwa wa tano alisema ndiyo, kuwa mizizi ya maneno ya lugha ya Kisambaa imeathiriwa na lugha nyingine zinazotumika pamoja nayo na aliitaja lugha ambayo imeiathiri mizizi ya maneno ya lugha ya Kisambaa ambayo ni lugha ya Kiswahili.

Mhojiwa wa sita alisema ndiyo, kuwa mizizi ya maneno ya lugha ya Kisambaa imeathiriwa na lugha nyingine zinazotumika pamoja nayo na aliitaja lugha ambayo imeiathiri mizizi ya maneno ya lugha ya Kisambaa ambayo ni lugha ya Kiswahili.

Mhojiwa wa saba alisema ndiyo, kuwa mizizi ya maneno ya lugha ya Kisambaa imeathiriwa na lugha nyingine zinazotumika pamoja nayo na aliitaja lugha ambayo imeiathiri mizizi ya maneno ya lugha ya Kisambaa ambayo ni lugha ya Kiswahili.

Mhojiwa wa nane alisema ndiyo, kuwa mizizi ya maneno ya lugha ya Kisambaa imeathiriwa na lugha nyingine zinazotumika pamoja nayo na aliitaja lugha ambayo imeiathiri mizizi ya maneno ya lugha ya Kisambaa ambayo ni lugha ya Kiswahili.

Mhojiwa wa tisa alisema ndiyo, kuwa mizizi ya maneno ya lugha ya Kisambaa imeathiriwa na lugha nyingine zinazotumika pamoja nayo na aliitaja lugha ambayo imeiathiri mizizi ya maneno ya lugha ya Kisambaa ambayo ni lugha ya Kiswahili.

Mhojiwa wa kumi alisema ndiyo, kuwa mizizi ya maneno ya lugha ya Kisambaa imeathiriwa na lugha nyingine zinazotumika pamoja nayo na aliitaja lugha ambayo imeiathiri mizizi ya maneno ya lugha ya Kisambaa ambayo ni lugha ya Kiswahili.

Mhojiwa wa kumi na moja alisema ndiyo, kuwa mizizi ya maneno ya lugha ya Kisambaa imeathiriwa na lugha nyingine zinazotumika pamoja nayo na aliitaja lugha ambayo imeiathiri mizizi ya maneno ya lugha ya Kisambaa ambayo ni lugha ya Kiswahili.

Mhojiwa wa kumi na mbili alisema ndiyo, kuwa mizizi ya maneno ya lugha ya Kisambaa imeathiriwa na lugha nyingine zinazotumika pamoja nayo na aliitaja lugha ambayo imeiathiri mizizi ya maneno ya lugha ya Kisambaa ambayo ni lugha ya Kiswahili.

Mhojiwa wa kumi na tatu alisema ndiyo, kuwa mizizi ya maneno ya lugha ya Kisambaa imeathiriwa na lugha nyingine zinazotumika pamoja nayo na aliitaja lugha ambayo imeiathiri mizizi ya maneno ya lugha ya Kisambaa ambayo ni lugha ya Kiswahili.

Mhojiwa wa kumi na nne alisema ndiyo, kuwa mizizi ya maneno ya lugha ya Kisambaa imeathiriwa na lugha nyingine zinazotumika pamoja nayo na aliitaja lugha

ambayo imeiathiri mizizi ya maneno ya lugha ya Kisambaa ambayo ni lugha ya Kiswahili.

Mhojiwa wa kumi na tano alisema ndiyo, kuwa mizizi ya maneno ya lugha ya Kisambaa imeathiriwa na lugha nyingine zinazotumika pamoja nayo na aliitaja lugha ambayo imeiathiri mizizi ya maneno ya lugha ya Kisambaa ambayo ni lugha ya Kiswahili.

Mhojiwa wa kumi na sita alisema ndiyo, kuwa mizizi ya maneno ya lugha ya Kisambaa imeathiriwa na lugha nyingine zinazotumika pamoja nayo na aliitaja lugha ambayo imeiathiri mizizi ya maneno ya lugha ya Kisambaa ambayo ni lugha ya Kiswahili.

Wahojiwa kumi na sita(16) ambao ni asilimia mia moja(100%) walitoa majibu yaliyolandana na yalikuwa sahihi. Kwa hiyo, kutokana na majibu haya mtafiti aliyafanyia kazi na kukubaliana na majibu haya kuwa ni kweli mizizi ya maneno ya lugha ya Kisambaa imeathiriwa na lugha ya Kiswahili ambayo inatumika pamoja nayo.

Swali la pili; Ni mizizi ipi ya maneno ya lugha ya Kisambaa iliyoathiriwa na lugha nyingine?. Swali lilikuwa na lengo la kutaka kupata mizizi ya maneno ya lugha ya Kisambaa iliyoathiriwa na lugha nyingine. Watafitiwa wote kumi na sita(16) ambao ni asilimia mia moja(100%) walitaja mizizi ya maneno ya Kisambaa iliyoathiriwa na lugha ya Kiswahili.

Mtafitiwa wa kwanza alitaja neno **nhuna** ambalo limeathiriwa na lugha ya Kiswahili na kuwa **zuta** kutokana na neno halisi la Kiswahili **vuta.**

Mtafitiwa wa pili alitaja neno **iza** ambalo limeathiriwa na lugha ya Kiswahili na kuwa **soo** kutokana na neno halisi la Kiswahili **njoo.**

Mtafitiwa wa tatu alitaja neno **ng'unda** ambalo limeathiriwa na lugha ya Kiswahili na kuwa **ima** kutokana na neno halisi la Kiswahili **lima.**

Mtafitiwa wa nne alitaja neno **homeea** ambalo limeathiriwa na lugha ya Kiswahili na kuwa **luusha** kutokana na neno halisi la Kiswahili **rusha.**

Mtafitiwa wa tano alitaja neno **togoa** ambalo limeathiriwa na lugha ya Kiswahili na kuwa **sifiaa** kutokana na neno halisi la Kiswahili **sifia.**

Mtafitiwa wa sita alitaja neno **mee** ambalo limeathiriwa na lugha ya Kiswahili na kuwa **maziwaa** kutokana na neno halisi la Kiswahili **maziwa.**

Mtafitiwa wa saba alitaja neno **hoya** ambalo limeathiriwa na lugha ya Kiswahili na kuwa **shoka** kutokana na neno halisi la Kiswahili **shoka.**

Mtafitiwa wa nane alitaja neno **hungo** ambalo limeathiriwa na lugha ya Kiswahili na kuwa **zani** kutokana na neno halisi la Kiswahili **jani.**

Mtafitiwa wa tisa alitaja neno **baa** ambalo limeathiriwa na lugha ya Kiswahili na kuwa **mlangoo** kutokana na neno halisi la Kiswahili **mlango.**

Mtafitiwa wa kumi alitaja neno **Zumbe** ambalo limeathiriwa na lugha ya Kiswahili na kuwa **Muungu** kutokana na neno halisi la Kiswahili **Mungu.**

Mtafitiwa wa kumi na moja alitaja neno **siya** ambalo limeathiriwa na lugha ya Kiswahili na kuwa **baabaa** kutokana na neno halisi la Kiswahili **barabara.**

Mtafitiwa wa kumi na mbili alitaja neno **mazundo** ambalo limeathiriwa na lugha ya Kiswahili na kuwa **maingu** kutokana na neno halisi la Kiswahili **mawingu.**

Mtafitiwa wa kumi na tatu alitaja neno **mghome** ambalo limeathiriwa na lugha ya Kiswahili na kuwa **damu** kutokana na neno halisi la Kiswahili **damu.**

Mtafitiwa wa kumi na nne alitaja neno **mbazi** ambalo limeathiriwa na lugha ya Kiswahili na kuwa **huuma** kutokana na neno halisi la Kiswahili **huruma.**

Mtafitiwa wa kumi na tano alitaja neno **mhungo** ambalo limeathiriwa na lugha ya Kiswahili na kuwa **kizui** kutokana na neno halisi la Kiswahili **kivuli.**

Mtafitiwa wa kumi na sita alitaja neno **tandiko** ambalo limeathiriwa na lugha ya Kiswahili na kuwa **buangeti** kutokana na neno halisi la Kiswahili **blangeti.**

Hivyo, kutokana na data ambazo wahojiwa wote wamezitoa ni sawa na asilimia mia moja(100%), hivyo majibu haya ni sahihi, kwa kuwa mtafiti aliwauliza watafitiwa wote wakatoa majibu yanayofanana.

Jedwali lifuatalo linathibitisha hilo, Jedwali 4:1

**Jedwali 4.1: Mizizi Katika Lugha ya Kisambaa**

| Na | Mizizi Asilia ya Maneno ya Kisambaa | Maneno ya Kisambaa Yaliyoathiriwa na Kiswahili | Maneno Asilia ya Lugha ya Kiswahili |
|---|---|---|---|
| 1 | ng'unda | Ima | Lima |
| 2 | Iza | Soo | Njoo |
| 3 | Homeea | Luusha | Rusha |
| 4 | Mee | Maziwaa | Maziwa |
| 5 | Hoya | Shoka | Shoka |
| 6 | Hungo | Zani | Jani |
| 7 | Baa | Mlangoo | Mlango |
| 8 | Zumbe | Muungu | Mungu |
| 9 | Siya | Baabaa | Barabara |
| 10 | Mazundo | Maingu | Mawingu |
| 11 | Mghome | Damu | Damu |
| 12 | Nhuna | Zuta | Vuta |
| 13 | Mbazi | Huuma | Huruma |
| 14 | Mhungo | Kizui | Kivuli |
| 15 | Tandiko | Buangeti | Blangeti |
| 16 | Togoa | Sifiaa | Sifia |

Uchanganuzi na ufafanuzi wa data uliongozwa na nadharia ya Mofolojia Leksika, ambapo data zilichanganuliwa kwa kuangalia uhusiano uliopo baina ya mofolojia na fonolojia na namna zinavyohusiana katika mchakato wa uambishaji/unyambulishaji, kwamba wakati wa mchakato huu sauti huathiriana ama kwenye mzizi/shina la neno au kwenye kiambishi na husababisha mabadiliko ya kiumbo.

Kwa mantiki hii, data zilipatikana kutokana na nadharia hii, ambapo imechambua mizizi na kuonyesha namna ambavyo imeathirika na kupata mabadiliko ya kiumbo na kuwa na umbo jipya na kwamba mizizi unapopata mabadiliko na neno zima hubadilika kwa kuwa huundwa na vipashio ambavyo vimepangwa kimsonge.

Na pia nadharia hii imesaidia kuonyesha jinsi ambavyo mizizi ya maneno ya lugha ya Kisambaa ilivyoathirika kiumbo(kimofolojia) na pia kimatamshi(kifonolojia) na

kwa uhakika zaidi yamekuwa na mwelekeo wa Kiswahili kiasi cha kuweza kueleweka kwa mtu yeyote yule hata ambaye si wa jamii ya Wasambaa.

Swali la tatu; Ni athari zipi zilizosababishwa na lugha nyingine kwenye lugha ya Kisambaa kutokana na mizizi ya maneno yake kuathiriwa? Swali lilikuwa na lengo la kutaka kupata athari zilizosababishwa na lugha nyingine baada ya kuiathiri mizizi ya maneno ya lugha ya Kisambaa.

Watafitiwa kumi na sita(16) ambao ni asilimia mia moja(100%) walitaja athari mbalimbali zilizosababishwa na athari za lugha ya Kiswahili katika lugha ya Kisambaa. Athari hizo zilizotolewa na watafitiwa wote ni hizi zifuatazo:

Kupotea kwa mizizi asilia ya maneno ya lugha ya Kisambaa, watafitiwa walisema kuwa hii ni kutokana na maneno ya lugha ya Kiswahili kuingizwa kwenye lugha ya Kisambaa na kusababisha kuyaathiri na kuwa na mwelekeo kabisa na ya lugha ya Kiswahili.

Matabaka katika jamii ya Wasambaa, hii ni kutokana na jamii ya Wasambaa kuwa na makundi ya wanaozungumza Kisambaa asilia na wale wanaozungumza Kisambaa chenye maneno yaliyoathiriwa na hii pia ni kutokana na kuchanganya lugha. Hii ni athari kubwa kwani katika kuwepo kwa matabaka ni vigumu lugha kuendelea kukua.

Uongeaji wa lugha ya Kisambaa isiyo fasaha, watafitiwa walieleza kuwa hii ni kutokana na wanajamii wengi wa jamii ya Wasambaa kutotumia maneno asilia ya lugha yao kutokana na kuchanganya maneno, hivyo kutokana na hali hii hujikuta

wanatumia maneno yaliyoathiriwa ambayo siyo fasaha na imewapelekea kutozungumza lugha yao kwa ufasaha.

Athari nyingine ambayo imeelezwa na watafitiwa ni lugha yao ya Kisambaa kupoteza ladha halisi, hii ni kutokana na utumikaji wa lugha ya Kisambaa na ya Kiswahili hivyo imepelekea watu kuyatumia maneno ya Kiswahili, kwa hiyo kutokana na hali hii imesababisha lugha ya Kisambaa kupoteza ladha yake halisi na kusababisha kupotea kwa maumbo na matamshi halisi ya maneno ya lugha yake.

Lugha ya Kisambaa kutokukua na kuendelea, hii ni athari nyingine iliyoelezwa na watafitiwa iliyosababishwa na athari ya lugha ya Kiswahili kwenye Kisambaa, watafitiwa walisema hii ni kutokana na Kisambaa kukosa watumiaji wengi kutokana na jamii ya Wasambaa kupenda kutumia lugha ya Kiswahili na kuvutiwa nayo na hatimaye kuyachukua maneno yake na kuyaingiza na kuyatumia kwenye lugha ya Kisambaa. Kwa hiyo, kutokana na hali hii imeifanya lugha ya Kisambaa kushindwa kuzalisha maneno yake mapya ambayo yanasababisha lugha kukua, hivyo, kutokana na hali hii imesababisha lugha hii isikue na kuendelea kama zilivyo lugha nyingine.

Hivyo, kutokana na data ambazo watafitiwa wote wamezitoa ni sawa na asilimia mia moja(100%), hivyo majibu haya ni sahihi, kwa kuwa mtafiti aliwauliza watafitiwa wote wakatoa majibu yanayofanana.

Data hizo hapo juu zinaonyesha jinsi ambavyo mizizi ya maneno ya Kisambaa ilivyoathiriwa na Kiswahili kutokana na kutumika pamoja na kusababisha iwe na

mwonekano sawa na Kiswahili kutokana na maneno ya Kiswahili kuingizwa na kutumika katika lugha ya Kisambaa.

Katika utafiti huu, asilimia mia moja (100%) ya watafitiwa wamekubali kuwa mizizi ya maneno ya lugha ya Kisambaa imeathiriwa na lugha nyingine zinazo tumika pamoja nayo ambazo ni Kiswahili. Kwa kiwango hiki inadhihirisha kuwa lugha nyingine zinaweza kuathiri lugha mama ya jamii husika.

Hivyo data hii ya utafiti huu inatoa tafsiri kwamba lugha ya Kisambaa imeathiriwa na lugha ya Kiswahili kutokana na kutumika pamoja nazo.

Pia mtafiti alitumia njia ya dodoso kwenye upatikanaji wa data na kuzichambua data kwa njia ya jedwali, watafitiwa wote kumi na sita(16) walitoa majibu kutokana na maswali mtafiti aliyoyauliza kwenye dodoso kama ifuatavyo:

**Jedwali 4.2 Mizizi Katika Lugha ya Kizigua**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. Swali | Je unadhani kuwa mizizi ya maneno ya lugha ya Kisambaa imeathiriwa na lugha nyingine zinazotumika pamoja nayo? (a) ndiyo, (b) hapana. | | |
| Dodoso (wahusika 16) | 16 (100%) | 0 (%) | Ndiyo |
| Majibu ya Jumla | | | Imeathiriwa |
| 2. Swali | Je wazawa wa Jamii ya Wasambaa wanapozungumza wanachanganya maneno ya kisambaa na Lugha nyingine? Jibu Ndiyo au Hapana. | | |
| | Majibu | | |
| Wahusika (16) | 16 (100%) | 0 (%) | Ndiyo |
| Majibu ya Jumla | | | Wanachanganya Maneno ya Lugha ya Kisambaa na Lugha nyingine wanapozungumza |
| 3. Swali | Je hali hii ya kuchanganya maneno ya Lugha ya Kisambaa na Lugha nyingine inaweza kuepukika? Ndiyo au Hapana | | |
| | 12 (75%) | 4 (25%) | Ndiyo |
| Majibu ya Jumla | | | Inaweza kuepukika |
| 1. Swali | Je unaamini kuwa mizizi ya Lugha ya kisambaa inaweza kupotea kutokana na athari za Lugha nyingine? Ndiyo au Hapana | | |
| | 14 (87.5%) | 2 (12.5%) | Ndiyo |
| Majibu ya Jumla | | | Inaweza kupotea |

Kutokana na data za kwenye dodoso ambazo watafitiwa wote wamezitoa ni sawa na asilimia 90.625% hivyo majibu haya ni sahihi. Kwakuwa mtafiti aliwauliza na watafitiwa wote wakatoa majibu yanayofanana kwa asilimia kubwa.

### 4.2.2 Mambo yaliyosababisha Lugha nyingine kuathiri mizizi ya maneno ya lugha ya Kisambaa.

Zipo sababu za msingi zinazoweza kusababisha mizizi ya maneno ya lugha ya kisambaa kuathiriwa na lugha nyingine nazo ni kama zifutazo; Mwingiliano wa makabila, elimu, wazawa kutopenda kutumia lugha yao, Ufanano wa baadhi ya mizizi ya maneno ya lugha za asili moja, Baadhi ya watu wa makabila mengine kupenda kutumia lugha ya Kisambaa, Kasumba ya kudharau lugha za jamii, na kuchanganya lugha**.**

Hivyo basi lengo la pili la utafiti huu lilikuwa ni kubainisha sababu zinazopelekea lugha nyingine kuathiri mizizi ya maneno ya lugha ya Kisambaa. Ili kupata sababu hizo mtafiti aliwauliza watafitiwa swali lifuatalo: Je ni sababu zipi zinazosababisha mizizi ya maneno ya lugha ya Kisambaa kuathiriwa na lugha nyingine? Kwa kuzingatia swali hili watafitiwa walitoa sababu za mizizi ya maneno ya Kisambaa kuathiriwa na lugha nyingine kama zifuatazo:

#### 4.2.2.1 Mwingiliano wa Makabila

Asilimia 96.875% ambao ni 31 ya watafitiwa 32 walieleza kuwa inapotokea kuwa na mchanganyiko wa makabila, huweza kusababisha lugha moja kuiathiri nyingine kutokana na kadri lugha hizo zinavyotumika pamoja. Na hatimaye maneno ya lugha

iliyopo kuathiriwa na lugha nyingine. Hata hivyo asilimia 3.125% ya watafitiwa walisema mwingiliano wa makabila hauwezi kusababisha lugha moja kuiathiri nyingine kwa sababu jamii ya watu asilia wanaongea lugha husika wapo.

Ni ushahidi wa kweli kuwa muingiliano wa makabila ni sababu tosha katika kuathiri mizizi ya lugha yoyote ile ikiwemo lugha ya Kisambaa ambayo imeathirika kutokana na muingiliano huo. Kama walivyosema watafitiwa kipindi cha mahojiano.

#### 4.2.2.2 Elimu

Watafitiwa 32 ambao ni asilimia 100% walieleza kuwa nyakati tulizonazo ni za maendeleo, hivyo lugha haitabaki kama ilivyokuwa bali inaendelea kubadilika. Kutokana na maendeleo ya kielimu wazawa huchanganya lugha wakati wa mazungumzo hivyo husababisha mizizi ya asili ya maneno yao kupata athari. Huwezi kukataa kuwa maendeleo ya elimu ni kichocheo kikubwa katika kuathiri mizizi ya maneno ya lugha moja na nyingine katika jamii mbalimbali. Hivyo, nina kubaliana na watafitiwa bila tashwishwi kuwa elimu inachangia kwa kiasi kikubwa kuathiri mizizi ya maneno ya lugha hususani lugha ya kisambaa.

Kutokana na watu kupata elimu na kuwa wamahiri wa lugha zaidi ya moja, husababisha wazawa kutumia zaidi ya lugha moja wakati wa mazungumzo. Mfano kiingereza na kisambaa, kifaransa na kisambaa au hata Kiswahili na kisambaa.

#### 4.2.2.3 Wazawa Kutopenda Kutumia Lugha Yao

Watafitiwa 32 ambao ni asilimia 100% walidai kuwa kutokana na kuwepo kwa lugha mbalimbali katika jamii yao, hususani lugha ya Kiswahili, wazawa hutumia lugha ya

Kiswahili ambayo imekuwa na nguvu katika jamiilugha hiyo, hivyo hupenda kutumia maneno ya lugha hiyo ya Kiswahili.

Wazawa wengi hususani jamii ya watu wasomi na vijana huwa hawapendi kuzungumza lugha yao ya asili, wakiamini kuwa wanajitambulisha katika jamii yao kama watu walio staarabika kwa kupata elimu za kigeni. Hii imepelekea watu hawa kutengeneza tabaka linalo itwa wasomi ndani ya jamii husika na tabaka linalo changia kwa kiasi kikubwa katika kuangamiza lugha yao na mizizi ya maneno ya lugha ya kisambaa.

#### 4.2.2.4 Ufanano wa Baadhi ya Mizizi ya Maneno ya Lugha za Asili Moja

Watafitiwa 32 ambao ni asilimia 100% walieleza kuwa lugha ya Kisambaa ni lugha ya kibantu, hivyo ina sifa na tabia zinazofanana na lugha nyingine za kibantu. Hivyo, maneno ya lugha hizi yanafanan kwa kiasi kikubwa. Ni kweli kuwa kuna mfanano mkubwa wa mizizi ya maneno ya lugha za asili moja hivyo hupelekea mizizi ya lugha hizo kuathiriana kwa namna moja au nyingine.

#### 4.2.2.5 Baadhi ya Watu wa Makabila Mengine Kupenda Kutumia Lugha ya Kisambaa

Watafitiwa 28 kati ya 32 ambao ni asilimia 87.5% walieleza jambo hili ili watambulike kama wao pia ni wazawa kwa kuwa wengi walifika Lushoto kipindi cha vita baina ya makabila yaliyohusisha jamii ya Wapare kutoka Same na Wataita kutoka Kenya. Na wengine walihamia kutafuta makazi kwa ajili ya mifugo yao. Asilimia (12.5%) ya watafitiwa ambao ni 4 kati ya 32 hawakubaliani na swala hili

kwakuwa makabila mengine kama Wakamba hawakupenda kutumia lugha ya kissambaa.

Hivyo ikapelekea kuathiri mizizi ya maneno ya lugha ya Kisambaa kutokana na kuchanganya na maneno ya lugha yao. Ni kweli kuwa watu wa makabila mengine hupenda kutumia lugha ya kisambaa pamoja na lugha yao mama hivyo kusababisha athari kwenye lugha ya kisambaa.

**4.2.2.6 Kasumba ya Kudharau Lugha za Jamii**

Katika kueleza sababu hii, watafitiwa wote 32 amabo ni asilimia 100% walisema kuwa wapo baadhi ya watu hasa vijana hawawezi kuzungumza lugha yao kutokana na kuathiriwa na kasumba ya kudharau lugha yao na kuona kuwa ni ushamba kuzungumza lugha yao na pia watadharaulika na kuonekana kuwa ni washamba na kupenda kutumia lugha za kigeni kama Kiingereza na pia kutumia Kiswahili, na hivyo kusababisha athari za lugha hii katika mizizi ya maneno ya Kisambaa.

Kundi kubwa la vijana wa kizazi hiki wanaozungumza lugha za kigeni wamekuwa na kasumba ya kudharau lugha yao mama hivyo kuathiri kwa kiwango kikubwa lugha ya kisambaa. 0mary, (1970), anasema kuwa lugha nyingi za kibantu zinafifia na hata kuwa hatarini kutoweka kutokana na watu hasa vijana kutojua thamani iliyobebwa na lugha hizo katika utambulisho wao katika nyanja mbalimbali.

**4.2.2.7 Kuchanganya Lugha**

Watafitiwa 30 kati ya 32 ambao ni asilimia 93.75% walieleza kuwa baadhi ya watu huchanganya lugha zaidi ya moja wanapozungumza, hii ni kutokana na watu

wengine kutoijua lugha yake ya asili vizuri na hivyo huchanganya maneno lugha ya asili na ile anayoifahamu vizuri, hivyo mtu anaweza akaanza kuzungumza. Asilimia 6.25% ya watafitiwa ambao ni 2 kati ya 32 hawakubaliani kwa kusema kuwa kuchanganya lugha sio lazima kama unaielewa lugha yako kwa ufasaha na umahili wa hali ya juu. Kisambaa, halafu akahamia kwenye Kiswahili na hatimaye kwenye Kiingereza.

Watu wengi ni wahanga wakubwa katika sababu hii ya kuchanganya lugha hivyo inapelekea kuathiri lugha hiyo ikiwa ni pamoja na mizizi ya maneno ya lugha husika. Ni vyema watu wakaongea lugha moja kwa ufasaha ili kudumisha na kuendeleza lugha hiyo.

### 4.2.3 Mbinu za Kutumika Ili Kuweza Kukabiliana na Athari za Lugha Nyingine Kwenye Mizizi ya Maneno ya Lugha ya Kisambaa

Ili Kupata mbinu hizo mtafiti aliwauliza watafitiwa swali lifuatalo: Je kwa mapendekezo yako ni mbinu gani zitumike ili kuweza kukabiliana na athari za lugha nyingine katika mizizi ya maneno ya lugha ya Kisambaa? Kutokana na swali hili watafitiwa walitoa mbinu mbalimbali za kutumia ili kukabiliana na athari za lugha nyingine kwenye mizizi ya maneno ya lugha ya Kisambaa kama ifuatavyo:

#### 4.2.3.1 Wazawa Kupenda Kutumia Lugha Yao

Utambulisho wa jamii/mtu umefungamana na vitu vingi vya kijamii ikiwemo lugha, utamaduni, desturi, mila, dini, imani, mavazi, siasa na uchumi. Hivi vyote vikizingatiwa kwa ujumla husaidia kubainisha sio tu utambulisho wa mtu au jamii, bali pia hufanya utambulisho huo ukubalike miongoni mwa jamii.

Kupenda kutumia lugha yako ya kikabila ni jambo la muhimu kwani lugha ya kikabila ni utambulisho mzuri ambao unakuonyesha asili yako halisi ya mahali ulipotokea. Kwakuwa lugha ni utambulisho mzuri katika jamii ni vyema watu wakawa mahiri katika kutumia na kuzungumza lugha zao za asili wakati wa mazungumzo.

Watafitiwa wote 32 ambao ni 100% walieleza kuwa ili kukabiliana na athari za lugha nyingine ni lazima watu wa kabila la Wasambaa wapende kutumia lugha yao kuliko kutumia lugha nyingine na kutilia mkazo wanajamii wazungumze zaidi lugha hii na mara kwa mara.

Ni wazi kuwa, lugha yoyote ili ikue ni lazima iwe na watumiaji wengi katika jamii husika hivyo, ili kisambaa kikue na kutoathiriwa katika mizizi ya maneno yake lazima wazawa wapende kutumia lugha yao.

#### 4.2.3.2 Kutochanganya Lugha

Moja ya changamoto kubwa kwenye matumizi ya lugha katika siku za leo ni uchanganyaji wa lugha wakati wa mazungumzo. Changamoto hii imeendelea kukua katika jamii mbalimbali kiasi kwamba na kabila la Wasambaa nao wameathirika na kasumba hii, hivyo kuathiri kwa kiwango kikubwa lugha yao ya kisambaa.

Watafitiwa wote 32 ambao ni 100% walieleza mbinu nyingine kuwa ili kukabiliana na athari za lugha nyingine ni kutochanganya lugha wakati wa uzungumzaji. Kwamba wazawa wazungumze tu Kisambaa hii itasaidia kuepuka kuchanganya lugha ya Kisambaa na nyingine.

Japokuwa ni vigumu kuepuka suala hili la kuchanganya lugha wakati wa mazungumzo kutokana na maendeleo ya kielimu, kitekinolojia, na muingiliano wanajamii mbalimbali katika maeneo mbalimbali ya nchi, bado ni vyema msisitizo ukatolewa kwa wazungumzaji/wazawa kuepuka kuchanganya lugha wakati wa mazungumzo.

#### 4.2.3.3 Kuwepo Kwa Sera ya Lugha ya Kisambaa

Sera ni muhimu sana katika kukuza, kuendeleza na kuitunza lugha yoyote ile duniani, sera hupelekea utungwaji wa sheria ambayo itaongoza matumizi ya lugha kikanuni na kimustakabali.

Hivyo basi watafitiwa walieleza kuwa ili kukabiliana na athari ni lazima kuwepo kwa sera ya lugha za kimakabila ikiwa ni pamoja na lugha ya Kisambaa ambayo itaiendeleza lugha hii kwa kuzifanyia kazi changamoto zinazoikumba lugha hii.

Mtazamo huu wawatafitiwa ni mzuri katika kutunza amali za lugha ya kisambaa na lugha nyigine za kibantu. Hivyo, nina kubaliana na mtazamo huu kuwa ni muhimu idara husika zikatengeza sera au kama sera hiyo ipo ni vyema msisitizo ukatolewa ilikuitumia sera hiyo katika kudumisha lugha za kibantu na kisambaa kimahususi.

#### 4.2.3.4 Kutolewa kwa Elimu

Watafitiwa 22 ambao ni asilimia 68.75% walishauri kuwa kuwepo na mpango mkakati wakutoa elimu kwa wazawa katika kutumia, kuendeleza na kukuza lugha ya kisambaa ili kuilinda na kuihifadhi kutoka kwenye muingiliano wa lugha nyingine

ilikuto athiri mizizi ya lugha ya kisambaa. 31.25% ambao ni sawa na watafitiwa 10 hawakusema chochote kuhusu swala la elimu.

Wazawa waelimishwe juu ya umuhimu wa kuzungumza lugha ya Kisambaa na faida ya uhifadhi wa lugha hii ili kuepuka athari za lugha nyingine kwenye Kisambaa. Hivyo basi, ni kweli kuwa elimu ni kitu cha msingi sana kutolewa ili watu wa jamii ya kisambaa waweze kupata mbinu sahihi za kutunza, kulinda na kuhifadhi mizizi ya lugha ya kisambaa.

#### 4.2.3.5 Kutopuuzia Matumizi ya Lugha ya Kisambaa

Watafitiwa wote 32 ambao ni asilimia 100% waliokubaliana na hoja hii walisema kuwa wazawa wanapaswa kutopuuzia matumizi ya lugha ya kisambaa katika mazungumzo kwenye shughuli mbalimbali za kijamii. Hivyo basi wazawa wanashauriwa kutoidharau lugha yao ili kuweza kuidumisha, kuikuza na kuiendeleza lugh hii kwa ajili ya vizazi vijavyo.

Pamoja na mitazamo mbalimbali ya watafitiwa inadhihirisha wazi kuwa ilikuepuka athari nyingine kwenye mizizi ya maneno ya lugha ya kisambaa wanajamii wana shauriwa kutopuuzia/kuzingatia matumizi sanifu ya lugha ya kisambaa.

## 4.3 Kupotea kwa Mizizi ya Maneno ya Kisambaa

Mizizi ya maneno ya lugha yoyote inaweza kupotea endapo kutakuwepo na kuathiriana kwa lugha nyingine kutokana na muingiliano wa lugha, hivyo basi ni vyema jambo hili likaangaliwa kwa jicho pevu ili kuhakikisha suala hili lisiweze kutokea katika lugha husika.

Asilimia tisini na nane (98%) ya watafitiwa walisema kuwa mizizi ya maneno ya lugha ya kisambaa inaweza kupotea kutokana na athari za lugha nyingine na asilimia 2% walisema haiwezi kupotea kwa sababu wazawa asilia wanao zungumza lugha asilia ya kisambaa bado wapo hivyo, ni vigumu mizizi hiyo ya maneno ya lugha ya kisambaa kupotea.

Pamoja na uhalisia kwamba asilimia kubwa ya watafitiwa walisema kuwa mizizi ya maneno ya lugha ya kisambaa inaweza kupotea kutokana na athari za lugha nyingine, ambayo ni sababu ya kweli kabisa, pia hatuwezi kudharau asilimia chache za watu walio kataa hoja hiyo kwa kusema kuwa mizizi ya maneno ya lugha ya kisambaa haiwezi kupotea endapo kama wazungumzaji halisi wa lugha ya kisambaa kama bado wapo.

Jambo la msingi la kuzingatia, ni vema kukawepo na msisitizo wa kuangalia sababu zote mbili kwa jicho kuntu ili kuhakikisha kuwa mizizi ya maneno ya lugha ya kisambaa haiathiriwi kwa na namna yoyote kwakuto zingatia sababu hizo za msingi.

## 4.4 Umuhimu wa Kuhifadhi Mizizi ya Maneno ya Lugha ya Kisambaa

Upo umuhimu mkubwa sana wa kuhifadhi mizizi ya lugha yoyote ile, ili kulinda, kuikuza, na kuiendeleza lugha hiyo.

Mzizi ni mojawapo kati ya vitu vya muhimu ambavyo hutazamwa katika lugha, na ni msingi muhimu katika uundaji wa maneno, japokuwa si maarufu kama neno lakini lazima uwepo pale. Hivyo maneno katika lugha hujibainisha kutokana na mizizi

iliyoundwa nayo, kwa kuwa mizizi ni kipengele muhimu katika lugha ambacho hujitokeza katika maumbo ya maneno.

Na pia kwa kawaida lugha nyingi za ulimwengu huwa zina mizizi. Hata hivyo, mizizi hubeba maana ya neno na huwa na umuhimu wa kimaana katika maneno yote ya lugha, na kitu kinachojitokeza wazi katika lugha ni maneno.

Watafitiwa asilimia mia moja(100%) walisema kuwa upo umuhimu wa kuhifadhi mizizi ya maneno ya lugha ya Kisambaa ili kuirithisha kwa vizazi vijavyo, ili waweze kujua mizizi asilia ya lugha yao na ili kuundia maneno mapya na hatimaye kuongeza msamiati wa lugha ya Kisambaa.

## 4.5 Hitimisho

Sura hii ilihusika na uwasilishaji na uchambuzi wa data zilizokusanywa uwandani, ambapo tumeona kwamba lugha ya Kisambaa imeathiriwa na lugha ya Kiswahili kwenye mizizi ya maneno yake.

Imeonyesha pia mizizi ya maneno ya Kisambaa iliyoathiriwa na Kiswahili. Pamoja na hivyo, inaonyesha athari za lugha nyingine kwenye mizizi ya maneno ya lugha ya kisambaa. Sababu za athari za lugha nyingine kwenye mizizi ya maneno kwenye lugha ya Kisambaa, mbinu za kuzuia athari za lugha nyingine kwenye lugha ya kisambaa, kupotea kwa mizizi ya maneno ya lugha ya Kisambaa na umuhimu wa kuhifadhi mizizi ya maneno ya lugha ya Kisambaa kwenye jamii ya wazungumzaji wa lugha ya Kisambaa.

# SURA YA TANO

# 5.0 MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.1 Utangulizi

Sura hii inakusudiwa kutoa muhtasari wa mambo muhimu kwa kila sura zilizotangulia ambayo yanaendana na malengo ya utafiti huu. Itatoa hitimisho la matokeo ya utafiti kuhusu Athari za lugha nyingine kwenye mizizi ya maneno ya lugha ya Kisambaa tangu mwanzo hadi mwisho wa utafiti kulingana na malengo ya utafiti. Na inaelezea mafanikio ya nadharia iliyotumika katka utafiti huu. Pia inaelezea mchango wa utafiti huu kitaaluma. Na kutoa mapendekezo juu ya maeneo yanayopaswa kufanyiwa utafiti zaidi na watafiti wengine kwenye tafiti zijazo na mwisho ni hitimisho.

## 5.2 Muhtasari

Huu ni utafiti wa uwandani uliofanyika Mkoa wa Tanga, Wilaya ya Lushoto katika kata ya Kwesimu. Sehemu hii ilichaguliwa kwa kuwa ndiko wanakoishi Wasambaa wengi wanaozungumza Kisambaa cha asilia.

Utafiti huu ni utafiti uliowasilishwa kwa njia ya maelezo na majedwali. Kama ilivyoelezwa awali utafiti huu ulihusu Athari za lugha nyingine kwenye mizizi ya maneno ya lugha ya Kisambaa. Ulilenga kuchunguza athari za lugha nyingine kwenye mizizi ya maneno ya lugha ya Kisambaa, kubaini lugha iliyoiathiri lugha ya Kisambaa. Pia, ilikuwa ni kubainisha mizizi ya maneno ya Kisambaa iliyoathiriwa na lugha nyingine zinazotumika pamoja nayo sababu zilizopelekea lugha nyingine

kuathiri mizizi ya maneno ya lugha ya Kisambaa na mbinu za kutumia ili kukabiliana na athari hizo.

Utafiti huu ni hatua muhimu mojawapo kwa kuwa utafiti huu unaonesha jinsi lugha mbalimbali za kibantu zinavyoweza kufanyiwa utafiti katika taaluma mbalimbali za lugha.

Sura ya Kwanza, katika utafiti huu imetoa maelezo ya maana ya Mofolojia kwa muhtasari kwa kuwa utafiti huu upo katika mtazamo wa taaluma ya mofolojia, maelezo hayo yanasaidia kujenga uelewa wa utafiti na pia imetoa maelezo kuhusu maathiriano ya lugha.

Katika utafiti huu imejadili usuli wa utafiti, tamko la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, mipaka na mawanda ya utafiti na kutoa hitimisho la sura ya kwanza. Kwa ufupi sura hii imefafanua nini hasa kimemsukuma mtafiti kufanya uchunguzi juu ya Athari za lugha nyingine kwenye mizizi ya maneno ya lugha ya kisambaa.

Sura ya Pili, katika sura hii mtafiti amefafanua nadharia ambayo ameitumia kuchambua mizizi ya maneno ya Kisambaa. Na ilihusu pia mapitio ya maandiko mbalimbali yanayohusu mizizi ya maneno. Mapitio yaliyopo katika sura hii yameeleza tu kwa ujumla mizizi ya maneno na jinsi inavyokuwa kwenye neno na maana inayobeba na kutolea mifano ya jumla inayoonyesha mizizi ya maneno hayo.

Hivyo mtafiti amedhihirisha kuwa kumekuwa na pengo kubwa katika sarufi ya lugha ya Kisambaa ambalo amejaribu kuliziba kwa kuchunguza athari za lugha nyingine kwenye mizizi ya maneno ya lugha ya Kisambaa.

Sura ya Tatu, imeonyesha mbinu zilizotumika kukusanyia data ya utafiti huu. Mbinu hizo ni pamoja na hojaji na mahojiano. Eneo la utafiti pia limebainishwa ambapo mtafiti amekusanya data yake katika kata ya Kwesimu Wilaya ya Lushoto, Tanga. Na kipengele kingine kilichojadiliwa ni populesheni lengwa ya utafiti.

Pamoja na hayo, mtafiti katika sura hii ameonyesha kipengelele cha sampuli na usampulishaji kinachojumuisha sampuli, usampulishaji na aina za usampulishaji, aina za data na kipengele cha mwisho ni cha mbinu za uchambuzi wa data na kutoa hitimisho la sura ya tatu.

Sura ya Nne, imeshughulikia uwasilishaji na uchambuzi wa data. Mtafiti ameonyesha lugha iliyoiathiri mizizi ya maneno ya lugha ya Kisambaa, na ameweza kubainisha mizizi ya maneno mbalimbali ya Kisambaa ambayo imeathiriwa na lugha ya Kiswahili. Mtafiti amefafanua athari zilizosababishwa na lugha ya Kiswahili kwenye lugha ya  Kisambaa kutokana na mizizi ya maneno yake kuathiriwa na Kiswahili.

Pia mtafiti amejadili sababu za athari za lugha nyingine kwenye mizizi ya maneno ya lugha Kisambaa, athari zenyewe na mbinu za kukabiliana na athari hizo. Na ni sura ambayo imeshughulikia mawasilisho ya data ambapo inatoa majibu ya maswali

yaliyotolewa na watafitiwa. Majibu yaliyotolewa yamejadiliwa vizuri na kuwezesha kufikia malengo yaliyowekwa.

Data zimekusanywa na kuchanganuliwa na hivyo kubainisha athari za lugha nyingine kwenye mizizi ya maneno ya lugha ya Kisambaa. Pia sura hii inadokeza sababu zilizotolewa na watafitiwa juu ya athari za lugha nyingine kwenye mizizi ya maneno ya Kisambaa.

Licha ya hayo, sura hii ya mwisho ambayo ni sura ya tano katika utafiti huu imetoa muhtasari, hitimisho na mapendekezo na matokeo muhimu ya utafiti huu kama yanavyoonekana hapo chini.

## 5.3 Matokeo ya Utafiti

Katika mchakato wa Kuchunguza athari za lugha nyingine kwenye mizizi ya maneno ya lugha ya Kisambaa, lengo kuu lilikuwa ni kuchunguza athari za lugha nyingine kwenye mizizi ya maneno ya lugha ya Kisambaa.

Malengo mahususi yalikuwa ni haya yafuatayo:

- Kubainisha mizizi ya maneno ya lugha ya Kisambaa iliyoathiriwa na lugha nyingine zinazotumika nayo.
- Kueleza athari za lugha nyingine kwenye mizizi ya maneno ya lugha ya Kisambaa.
- Kubaini mambo yaliyosababisha Lugha nyingine kuathiri mizizi ya maneno ya lugha ya Kisambaa.

Maswali ya utafiti huu yalikuwa kama ifuatavyo:

- Ni mizizi ipi ya maneno ya lugha ya Kisambaa iliyoathiriwa na lugha nyingine zinazotumika nayo?
- Ni athari zipi zilizosababishwa na lugha nyingine kwenye mizizi ya maneno ya lugha ya Kisambaa?
- Ni mambo yapi yaliyosababisha Lugha nyingine kuathiri mizizi ya maneno ya lugha ya Kisambaa?

Kwa hiyo basi, katika mchakato wa kukusanya na kuchanganua data, utafiti huu umeona kuwa mizizi ya maneno ya lugha ya Kisambaa imepata athari ya lugha mbalimbali za kibantu kwani kwao lugha ya kwanza ni Kisambaa na ya pili ni Kiswahili.

Lugha ya Kiswahili ndio hasa imeathiri mizizi ya maneno ya lugha ya Kisambaa kwa kiwango kikubwa sana kuliko lugha nyingine zinazotumika pamoja na Kisambaa. Hivyo kuna baadhi ya maneno ambayo wanayatumia katika lugha ya Kisambaa imetokana na lugha nyingine. Malengo yaliyowekwa katika utafiti huu yaliyotajwa hapo juu kwa hakika yamefanikiwa.

Lengo la kwanza ambalo ni *"Kubainisha mizizi ya maneno ya lugha ya Kisambaa iliyoathiriwa na lugha nyingine zinazotumika nayo",* kutimizwa kwa lengo hili kumefanikiwa katika kipengele cha uwasilishaji na uchambuzi kwa kubainisha athari za lugha nyingine kwenye mizizi ya maneno ya Kisambaa. Data inaonyesha kuwa mizizi ya maneno ya lugha ya Kisambaa imeathirika na kupata mabadiliko ya

kimofofonolojia (kimatamshi/kifonolojia na kiumbo/kimofolojia) na mabadiliko ya kisemantiki/kimaana, hii ni kutokana na sababu ya mizizi ya neno kupachikwa viambishi vinavyofanya mzizi kutoka katika uasilia wake na kuwa na mwonekano mwingine wa kiumbo(kimofolojia) na pia kubadilika katika matamshi yake(kifonolojia). Mabadiliko hayo yamesababishwa na mwingiliano wa lugha. Katika kipengele cha uwasilishaji na uchambuzi athari za lugha nyingine kwenye mizizi ya maneno ya lugha ya Kisambaa zimebainishwa. (sura ya nne).

Lengo la pili ambalo ni "*Kueleza athari za lugha nyingine kwenye  mizizi ya maneno ya lugha ya Kisambaa*", Lengo hili limefanikiwa kwa kueleza athari za lugha kwenye  mizizi ya maneno ya lugha ya Kisambaa.

Lengo la tatu la utafiti huu lilikuwa ni *"Kubaini mambo yaliyosababisha Lugha nyingine kuathiri mizizi ya maneno ya lugha ya Kisambaa".* Hapa katika mjadala wetu wa sura ya nne tumeona kuwa lengo hili limetimizwa kwa kubainisha sababu zilizosababisha lugha nyingine kuathiri mizizi ya maneno ya lugha ya  Kisambaa. kwa kuwa athari katika lugha hazitokei tu kiholela au  kwa kubahatisha bali hutokea kutokana na mambo/sababu mbalimbali kama zilivyojadiliwa katika sura ya nne.

## 5.4 Mafanikio ya Nadharia

Nadharia iliyotumiwa katika utafiti huu ni nadharia ya mofolojia leksika. Nadharia kama ufafanuzi ulivyotolewa kuwa inaonyesha uhusiano wa maumbo ya maneno na sheria zinazo dhibiti maumbo hayo, kwa maana kwamba viambishi (mofimu) vinapopachikwa katika mizizi ya neno hupangwa kidarajia.

Na pia, nadharia hii hufafanua jinsi mofolojia na fonolojia zinavyohusiana katika mchakato wa uambishaji na/au unyambulishaji, kwamba wakati wa uambishaji au unyambulishaji kuna sauti zinaathirika ama kwenye mzizi/ au shina la neno au kwenye kiambishi chenyewe na hivyo kusababisha mabadiliko ya kiumbo, ulisaidia katika kubainisha athari za lugha nyingine kwenye mizizi ya maneno ya lugha ya Kisambaa kwa kuonyesha namna ambavyo mizizi ya Kisambaa imeathiriwa na kupata mabadiliko kutoka katika umbo(kimofolojia) lake la asili na kupata umbo lingine na pia imepata mabadiliko ya kimatamshi(kifonolojia). Kwa kuwa utafiti huu ulijikita katika mizizi ya maneno ya lugha ya kisambaa na kutumia msingi wa taaluma ya mofolojia.

Nadharia hii imesaidia kuimarisha na kufanikisha utafiti huu, kwa kuwa mzizi ndio msingi wa uundaji wa maneno katika lugha yoyote ile.

## 5.5 Mchango wa Utafiti

Utafiti huu unatoa mchango katika nyanja ya isimu hususani katika taaluma ya mofolojia, katika kudhihirisha kuwa mzizi ni sehemu muhimu katika lugha, na ni msingi muhimu katika uundaji wa maneno, kwa kuwa maneno katika lugha hujibainisha kutokana na mizizi iliyoundwa nayo.

Na pia utasaidia kuweka wazi historia ya lugha ya kisambaa, mizizi ya maneno ya lugha ya kisambaa na maana zake.

Utafiti huu utasaidia sana katika kuendeleza, kukuza na kuhifadhi misingi ya mizizi ya maneno ya lugha za kibantu katika jamii husika.

Utafiti huu unaweza kutumiwa na watafiti wengine wanao soma au kutafiti masuala mbalimbali katika isimu ya lugha ya Kiswahili au lugha nyingine za kibantu na kadhalika.

Utafiti huu unaweza kutumika katika shule za msingi, sekondari, na hata vyuo vya elimu ya juu katika kukuza na kuendeleza lugha ya Kiswahili na lugha nyingine.
Utafiti huu unaweza kutumiwa na mashirika mbalimbali yanayo jishughulisha na maswala ya lugha duniani ili kutoa msingi sahihi wa kuthamini mizizi ya maneno ya lugha ya kisambaa na lugha nyingine.

## 5.6 Mapendekezo

Kwa hakika hakuna utafiti uliofanyika ukawa ndio umemaliza kila kitu na ndio maana kwa kawaida matokeo ya utafiti wowote yanaanzisha tatizo la utafiti mwingine. Utafiti huu ulijikita katika mtazamo wa mofolojia katika kipengele cha mizizi ya maneno ya Kisambaa, Kwa kuchunguza athari za lugha nyingine kwenye mizizi ya maneno ya lugha ya Kisambaa. Hivyo kuna haja ya utafiti kama huu kufanywa kwenye lugha nyingine za kibantu.

Kwa upande mwingine utafiti unaweza kufanywa/kujikita katika kulinganisha na kulinganua mfanano wa mizizi ya maneno katika Kiswahili na lugha zingine za kijamii.

Pia utafiti unaweza kufanywa kwenye vipengele vingine muhimu vya maumbo ya maneno ambavyo ni viambishi na mashina. Utafiti wa namna hii pia unaweza

kufanyika kwenye taaluma nyingine za isimu kwa kuchunguza athari la lugha nyingine kwenye maana, matamshi, muundo katika lugha zao za asili.

## 5.7 Hitimisho

Sura hii ilihusu hitimisho na mapendekezo ambapo, kwanza ilianza na utangulizi uliodokeza vipengele muhimu katika sura nzima. Sehemu iliyofuata ni muhtasari unaodokeza kwa ufupi mambo muhimu yaliyojadiliwa katika sura zilizotangulia za tasnifu hii. Sehemu nyingine inatoa mapendekezo ya tafiti zijazo na mwisho ni hitimisho.

# MAREJEO

Abel, E. (2012). Matumizi ya Majina ya Ukoo katika Utambulisho wa Jamii ya Wasambaa. (Tasnifu ya M.A.Kiswahili). Taasisi ya Taaluma za Kiswahili. MAKAVAZI. Chuo Kikuu cha Dar es Saalam.

Bauer, L. (1983). *English Word- Formation*. Cambridge: Cambridge University Press.

Besha, R. M. (1985). A study of Tense and Aspect in Shambala. (Phd Thesis). Taasisi ya Taaluma za Kiswahili. MAKAVAZI. Chuo Kikuu cha Dar es Saalam.

Besha, R. M. (1989). "Mood in Bantu Languages: An Exemplification from Shambala." In *ILCAA* Vol. 5 *Studies in Tanzania Languages*. Tokyo: Institute for the study of Languages and Cultures of Asia and Africa Dammann, E (1968), Sprachliche Bemuehungen Von Betheler Missionaren und das Schambala in Ostafrikanische studies 8.

Bloomfield, L. (1888). *Language*. New York: Holt.

Charwi, M. Z. (2013). Vitenzi vya kibantu. Katika Kioo cha Lugha, (*Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili*, Juz. 11, 60), Idara ya Kiswahili (TATAKI) – MAKAVAZI. Chuo Kikuu cha Dar es Saalam.

Chava, N. & David, N. (1981). *Research Methods in Social Sciences*. London: St. Martin’s Press.

Coulmas, F. (ed.) (1965), *Sociolinguistics*. The Hague: Mounton.

David, O. (1982). *“Tonal Phenomena in Kishambala”.* Katika Studies in African Linguistics 13, 177-208.

Enon, J. (1998). *Education Research, Statistic and Measurements*. Kampala: Makerere University Press.

Goldsmith, J. (1990). *Autosegmental and Metrical Phonology*. Oxford: Basil Blackwell.

Good, J. (2005). *"Reconstructing Morpheme Order in Bantu*: The case of Causativization and Applicativization". Katika Diachronica 22, 3-57.

Habibu, N. (2011). Muundo wa Kirai Kitenzi katika Lugha ya Kisambaa.(Tasnifu ya M.A.Kiswahili). Taasisi ya Taaluma za Kiswahili. MAKAVAZI. Chuo Kikuu cha Dar es Saalam.

Hartman, R. (1972). *Dictionary of Language and Linguistics*. London: Applied Science Publishers.

Idarus. (2005). *Athari za lugha katika lugha ya Kiswahili*. Dar es Salaam: TUKI.

Jilala, H. (2016). *Nadharia za Tafsiri, Ukalimani na Uundaji wa Istilahi*. Dar es Salaam: Daud Publishing Company Limited.

Johannes, G. (2007). "The Ki-Nata Noun Structure". Unpublished M.A Dissertation. University of Dar es Salaam.

Johannes, G. (2011). "Mkanganyiko wa dhana za Mzizi, Kiini na Shina katika Mofolojia ya Kiswahili".(Katika *Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili*, Juz. 74, 12-24). Taasisi ya Taaluma za Kiswahili. MAKAVAZI. Chuo Kikuu cha Dar es Saalam.

Kahigi, K. K. (2009). "Unyambulishi wa Nomino na Vitenzi katika Kikahe". Katika *Kioo cha Lugha,* Juz. 7, 1-10.

Kahigi, K. K. (2003). *"The Sisumbwi Noun: Its Classes and Derivation"*. (In Occasional Papers in Linguistics. No.1.pp. 1-86). University of Dar es Salaam: LOT Publications.

Kaoneka, S. (2009). Unyambulishaji wa kitenzi katika Kisambaa, (Katika Kioo cha Lugha, *Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili*, Juz. 11, 60). Taasisi ya Taaluma za Kiswahili. MAKAVAZI. Chuo Kikuu cha Dar es Saalam.

Katamba, F. (1993). *Morphology*. London: Macmillan Press Limited.

Kiango, J. G. (2000). Bantu Lexicography: a Critical Survey of the principles and Process of Constructing Dictionary Entries. Institute for the study of Languages and Cultures of Asia and Africa Tokyo University of Foreign Studies, Japan.

Kihore Y. M. (1999). *Sarufi Miundo ya Kiswahili Sanifu (SAMIKISA),* Sekondari na Vyuo. TUKI, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Kihore Y. M. (1994). A study of the Syntax of Kiswahili Verbs. (Phd Thesis). Taasisi ya Taaluma za Kiswahili. MAKAVAZI. Chuo Kikuu cha Dar es Saalam.

Kihore Y. M. (2004). *Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu (SAMAKISA)*. Dar es Salaam: TUKI.

Kombo, D. K., & Tromp, D. L. (2006). *Proposal and Thesis Writing*: *An Introduction*. Nairobi: Paulines Publication Africa.

Kothari, C. R. (2014). *Research methodology: Methods and techniques*. New Delh: New Age International Publishers.

Kothari, C. R. (1985). *Research Methodology, Methods and Techniques*. New Delhi: Wiley Easton Limited.

Kothari, C. R. (2004). *Research Methodology, Methods and Techniques,* New Delhi: Dharmesh Printers.

Kothari, C. R., & Garg, G. (2014). *Research Methodology, Methods and Techniques:* Third Edition. New Delhi: New Age International (P) Limited Publishers.

Languages of Tanzania Project (LOT) (2008). *Atlasi ya Lugha za Tanzania*. Dar es Salaam, Chuo Kikuu cha Dar se Salaam.

Lyons, J. (1968). *Introduction to Theoretical Linguistics*. Cambridge: Cambridge University Press.

Malangwa, S. P. (2011). "Athari na Dhima ya Vijenzi Nomino katika Vitenzi vya Kiswahili". Katika *Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili*, Juz. 74, 28-40). Taasisi ya Taaluma za Kiswahili. MAKAVAZI. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Masebo, J. A & Nyangwine, N. (2002), *Nadharia ya Lugha, Kiswahili 1, Kidato cha 5 na 6*. Dar es salaam: Nyambari Nyangwine Publisher.

Massamba, D. P. B. (1990). *Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha*. Dar es salaam: TUKI.

Massamba, D. P. B. (2004). *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha*. Dar es Salaam: TUKI.

Matinde, R.S. (2012). *Dafina ya Lugha; Isimu na Nadharia, Sekondari, Vyuo vya kati na Vyuo Vikuu*. Mwanza: Serengeti Educational Publishers (T) Ltd.

Mbaabu, I. (2007). *Historia ya Usanifishaji wa Kiswahili*. Chuo Kikuu cha Dar es Saalam: TUKI.

Meeussen, A. E. (1967). *Bantu grammatical reconstructions*. Tervuren: Tervuren.

Mekacha, D. (2011). *Isimujamii: Nadharia na Muktadha wa Kiswahili*. Dar es Salaam: TATAKI.

Mekacha, R.D.K. (2011). *Isimu Jamii; Nadharia na Muktadha wa Kiswahili,* Minocity: Osaka University of Foreign studies.

Mgullu, R. S. (2002). *Mtaala wa Isimu; Fonetiki, Fonolojia na Mofolojia ya Kiswahili.* Nairobi: Longhorn.

Mochiwa, Z. (2008). *Msamiati wa Kizigula-Kiswahili-Kiingereza [Zigula-Swahili-English lexicon]*. Languages of Tanzania Project (LOT). University of Dar es Salaam.

Mohamed, M. A. (2001). *Modern Swahili Grammer*. Nairobi: Sitima Printers and Stationery Ltd.

Mohamed, M. A. (2006). *Sarufi Mpya*. Dar es Salaam: Press and Publicity Centre.

Msanjila, Y.P (2003). "Kushuka kwa Hadhi ya Lugha za Kijamii nchini Tanzania": *Nordic Journal of African Studies*, 12(3), 296-309. Dar es Salaam, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Muzale, H. R. T. (2008). *"Occasional Papers in Linguistic*: Dar es Salaam: University of Dar es Salaam.

Nurse, D. (1979). "Description of Sample Bantu Languages of Tanzania*".* In *Journal of African Languages*, 5(1).

Omary, C. K. (1970). "Person Names in Sociol- cultural contex": Jarida la Kiswahili la Chuo cha Uchunguzi wa Lugha ya Kiswahili (*Journal of the Institute of Swahili Research*), 40/2, sep, 1970, Dar es Salaam, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Peterson, R. (2008). "Baadhi ya vipengele vya uambatizi wa vitenzi katika Kishambala". Katika *Kioo cha Lugha*, Juz 7,12-24. Taasisi ya Taaluma za Kiswahili. MAKAVAZI. Chuo Kikuu cha Dar es Saalam.

Polome, E. C. (1967). *Swahili language Handbook.* 1717 Massachusetts A Venue: Centre for Applied Linguistics.

Pride, J. B. & Holmes, J. (1972). *Sociol Linguistic.* London: Penguin Books Ltd, Harmond Sworth.

Radford, A na wenzake (2002), *Linguistic, An Introduction*. Cambridge: Cambridge University Press.

Ralf, F. (1998). *Sociolinguistic of Society*. New York: Basil Blackwell Inc.

Rugemalira, J. M. (2005). *A Grammar of Runyambo*. Dar es Salaam: Language of Tanzania Project (LOT), University of Dar es Salaam.

Taasisi ya Elimu, (1996). *Kiswahili Kidato cha pili*. Oxford University Press.

Thomason. S. K. (2001). *Language Contact*. Edinburgh: University Press.

Ullman, S. (1964). *Semantics an Introduction to Science of Meaning*. Oxford: Basil Blackwell.

Wesana-Chomi, E. (2003). *Kozi Fupi Tangulizi katika Sarufi Maumbo ya Kiswahili*. Sebha: Chuo Kikuu cha Sebha.

Whitney, W. D. (1989). *Sanskrit Grammar*. Cambridge, Mass: Harvard University Press.

William. L. A. (1913). *Athari za Sheng katika lugha ya Kiswahili*. www.academic.edu/9499200/.

Yukawa, Y. (1984). *A Classified Dictionary of the Sambaa Language*. Tokyo: Institute for the Study of Language and Cultures of Asia and Africa.

# VIAMBATANISHO

## KIAMBATANISHO A- DODOSO

**CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA**

**KITIVO CHA SANAA NA SAYANSI YA JAMII**

**IDARA YA ISIMU NA TAALUMA ZA FASIHI**

Dodoso hii ni kwa ajili ya kupata taarifa kuhusu mizizi ya maneno ya lugha ya Kisambaa.

Unatakiwa ujibu maswali yafuatayo kadri ya uelewa wako.

Tafadhali usiandike jina lako katika karatasi hii.

**SEHEMU A**

Jibu maswali yafuatayo:

Weka alama ya vema kwenye jibu sahihi ndani ya kisanduku.

(1) Umri wako

(a) 15-20

(b) 21-30

(c) 31-45

(d) 46-60

(e) 61-75

(2) Jinsia yako

(a) Kike

(b) Kiume

(3) Kiwango cha Elimu

(a) Msingi

(b) Sekondari

(c) Chuo

(d) Elimu nyingine

(4) Mafunzo

(a) Cheti

(b) Stashahada

(c) Shahada

(d) Mafunzo mengine

(5) Unazungumza lugha gani?____________

(6) Unaweza kuzungumza lugha nyingine?_________

(7) Zitaje lugha hizo unazoweza kuzizungumza___________, ___________, ____________, ______

(8) Mahali ulipozaliwa

(a) Kijiji________

(b) Wilaya________

(c) Mkoa_________

**SEHEMU B**

(9) Lugha yako ya kwanza ni ipi?

(a) Kisambaa (b) Kiswahili

(10) Lugha yako ya pili ni ipi?

(a) Kiswahili (b) Kisambaa

(11) Ni lugha gani unayoitumia zaidi kwenye mawasiliano yako ya kila siku?

(a) Kisambaa (b) Kiswahili (c) Kiingereza

**SEHEMU C**

(12) Je wazawa wa jamii ya Wasambaa wanapozungumza wanachanganya maneno ya Kisambaa na ya lugha nyingine?

(a) Ndiyo (b) Hapana

(13) Je hali hii ya kuchanganya maneno ya lugha ya Kisambaa na ya lugha nyingine yameathiri mizizi ya maneno ya lugha ya Kisambaa?

(a) Ndiyo (b) Hapana

Endapo jibu lako ni ndiyo taja mizizi ya maneno ya Kisambaa iliyoathiriwa na lugha nyingine na taja lugha hiyo iliyoiathiri lugha ya Kisambaa

| **Na** | **Mzizi asilia wa maneno ya Kisambaa** | **Mzizi wa maneno ulioathiriwa** | **Maneno yalivyo ya lugha iliyoiathiri** |
|---|---|---|---|
| 1 | | | |
| 2 | | | |
| 3 | | | |
| 4 | | | |
| 5 | | | |
| 6 | | | |

(14) Je hali hii ya kuchanganya maneno ya lugha ya Kisambaa na nyingine inaweza kuepukika?

(a) Ndiyo (b) Hapana

(15) Kwa mapendekezo yako kifanyike nini ili kuepuka hali hii ya kuchanganya maneno ya lugha ya Kisambaa na lugha nyingine?

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

**SEHEMU D**

(16) Je unaamini kuwa mizizi ya maneno ya lugha ya Kisambaa inaweza kupotea kutokana na athari za lugha nyingine?

(a) Ndiyo (b) Hapana

Toa maelezo

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

**SEHEMU E**

(17) Je unadhani zipo sababu zinazopelekea lugha nyingine kuathiri mizizi ya maneno ya lugha ya Kisambaa?

(a) Ndiyo (b) Hapana

**KIAMBATANISHO B- MAHOJIANO**

**CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA**

**KITIVO CHA SANAA NA SAYANSI YA JAMII**

**IDARA YA ISIMU NA TAALUMA ZA FASIHI**

**MWONGOZO WA MASWALI YA MAHOJIANO KUHUSU ATHARI ZA LUGHA NYINGINE KWENYE MIZIZI YA MANENO YA LUGHA YA KISAMBAA**

**SEHEMU A**

Jibu maswali yafuatayo:

Weka alama ya vema kwenye jibu sahihi ndani ya kisanduku.

1. (1)Umri wako

   (f) 15-20

   (g) 21-30

   (h) 31-45

   (i) 46-60

   (j) 61-75

2. Jinsia yako

   (c) Kike

   (d) Kiume

3. Kiwango cha Elimu

   (e) Msingi

   (f) Sekondari

   (g) Chuo

(h) Elimu nyingine

4. Mafunzo

   (a) Cheti

   (b) Stashahada

   (c) Shahada

   (d) Mafunzo mengine

5. Unazungumza lugha gani? ____________

6. Unaweza kuzungumza lugha nyingine? _________

7. Zitaje lugha hizo unazoweza kuzizungumza___________, ___________, ____________, _______

8. Mahali ulipozaliwa

   (a) Kijiji ________

   (b) Wilaya ________

   (c) Mkoa _________

**SEHEMU B**

9. Je unadhani kuwa mizizi ya maneno ya lugha ya Kisambaa imeathiriwa na lugha nyingine zinazotumika pamoja nayo?

   (a) ndiyo (b) hapana

Kama jibu lako ni ndiyo taja lugha hiyo/hizo.

10. Ni mizizi ipi ya maneno ya lugha ya Kisambaa iliyoathiriwa na lugha nyingine? Taja

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

11. Ni sababu zipi zinazopelekea lugha nyingine kuathiri mizizi ya maneno ya lugha ya Kisambaa?

……………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………